# MAKONGAMANO

Asante sana. Mungu akubariki ndugu.

2 Ni majaliwa makubwa kurudi tena, usiku wa leo, katika nyumba ya Bwana kutumika pamoja nawe ndugu na dada katika imani moja ya thamani ya Bwana Yesu. Nafikiri mengi yake yalikuwa ni sehemu yangu jana usiku ya labda kidogo kuwashikilia muda mrefu kupita kiasi. Nina si—sifa za kufanya ibada ndefu. Sijapata kufanya wowote mrefu kuliko usiku kucha. Kamwe sijachukua muda mrefu zaidi. Kidogo naja pamoja na mtume Paulo wakati alipohubiri usiku kucha naye yule mvulana akaanguka kutoka roshani akafa. Ndipo akaulaza mwili wake juu yake naye huyo mvulana akafufuka.

3 Kwa hiyo, mtu fulani aliniambia, akasema, "Ndugu Branham, kidogo u—unazungumza muda mrefu kupita kiasi." Vema, ni—nina mengi sana ya kuzungumzia na, naam, ka—kamwe siwezi kuyatoa yote kwa wakati mmoja. Ninaninii tu . . . Tangu Kristo kunijaza kwa Uwepo Wake, mbona, nimekuwa tu na mengi sana ya kusema juu yake.

4 Na kwa hiyo usiku wa leo tutajaribu kuwaachilia mtoke mapema, kwa sababu ninawazia juu ya heshima kwa ajili ya wale inaowabidi kwenda mbali, na inawabidi kwenda kazini, na kadhalika. Labda baadaye kidogo katika juma tutarefusha tu kidogo zaidi.

5 Basi jana jioni tulikuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa, ama kile tunachoita . . . mara nyingi inajulikana kama "ibada ya uponyaji." Hakika hatuninii . . . tunajua hatumponyi mtu yeyote, bali tunawaombea tu. Wala sijawahi kumponya mtu yeyote bado, bali bila shaka nimepata majibu makubwa ya maombi, tukimwona Bwana, Yeye huwaponya wagonjwa. Na kwa hiyo hiyo ndiyo sababu nipo hapa, kujaribu kushiriki pamoja nanyi kwenye mambo haya.

6 Wala si kwa kuponywa kwa mwili tu, bali kuponywa kwa nafsi pia, ambako ni muhimu sana kuliko kuponywa kwa mwili. Sasa, inawezekana kwamba kama ukiishi muda mrefu kutosha utakuwa mgonjwa tena, kwa sababu ugonjwa . . . Biblia ilisema, "Mateso ya mwenye haki ni mengi, bali Mungu humkomboa nayo yote." Kwa hiyo tunayo mateso mengi yaliyoahidiwa, bali ukombozi kutoka kwayo.

7 Katika majadiliano wakati marehemu Jack Coe . . . Huenda wengi walimfahamu. Yeye alikuwa rafiki yangu msiri sana. Niliwazia sana juu ya Ndugu Jack. Naye alikuwa na ninii sana, samahani kwa hili tamshi, kama imani ya kulazimisha kushikilia tu kwa ajili ya uponyaji. Na yeye angeninii . . . mtu fulani angekuja na mikongojo, alikuwa amejiwekea shoka ama

kitu fulani pale, yeye angeikatakata ama kuivunjilia mbali, kabla hata hajawaombea. Hakuwa aondoke na mikongojo hiyo tena, yeye . . . um-hum, kama hawangeweza kutembea waende, wangetambaa hata watakapopata imani ya kutosha ku . . .

8 Naye alikuwa na fuawe ndogo na nyundo zimewekwa pale, ndipo mtu angekuja amevaa miwani akaombewe, kwa ajili ya macho yao, angenyosha mkono na kuitoa, na kuivunja-vunja kwa fuawe, aitupe upande mmoja.

9 Kwa hiyo akaingia katika shida fulani huko Florida. Shetani alimwekea mtego akapata mtoto ambaye alimtoa magango. Hakika mnajua hiyo hadithi. Kasisi Gordon Lindsay alikuwa huko chini mahakamani wakati hakimu aliposema, "Ati unadai mvulana huyo ameponywa?"

Ndipo Ndugu Jack akasema, "Yeye aliponywa."

"Loo," akasema, "hakuna kitu kama hicho."

Kasema, "Nilipoyaondoa magango kutoka kwake, yeye alitembea akavuka jukwaa. Alisema aliponywa."

10 Kasema, "Sasa, kama unaweza kutoa Andiko moja ambapo Mungu aliwahi kufanya kitu kama hicho, angeponywa hapa, ama kitu fulani, nao utadumu tu dakika moja, mbona, niko radhi kuifutilia mbali."

Ndugu Lindsay akasimama, kasema, "Ninaweza kutoa Andiko."

Kasema, "Hebu tulisikie."

11 Kasema, "Usiku mmoja kwenye bahari yenye tufani, Yesu alimwambia Petro, alikuja Kwake akitembea juu ya maji; mradi tu alitembea, alikuwa juu ya maji kama alivyoamini; bali alipokuwa tayari kutokuamini, akazama."

12 Kwa hiyo hiyo ni kweli. Kwa hiyo hakimu angeweza kuifutilia mbali hiyo kesi. Kusingekuwa na la zaidi juu yake. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona, a—alikuwa—alikuwa, mradi tu alikuwa akitembea alikuwa sawa; bali alipoanza kutilia shaka, huyo akazama.

13 Na huo ndio muda uponyaji wa kiungu unaodumu: kadiri unavyouamini. Na huo ndio muda wokovu udumuo: kadiri tu unavyouamini.

14 Mtu fulani aliniambia wakati fulani uliopita, kasema, "Ndugu Branham, sijali kile ungaliweza kutoa, yale ungesema, ama mtu mwingine yeyote, ambaye . . . Huenda ukawafufua watu kumi waliokufa, na kumfanya kila kiwete kutembea," kasema, "Ningali ninaninii . . . nisingeamini hilo."

15 Nikasema, "Hakika usingaliamini. Halikuwa kwa ajili ya wasioamini; lilikuwa ni kwa wale tu wanaoamini." Hivyo tu. Ni—ni kwa ajili tu ya waaminio.

16 Yesu alisema "Kwa hao waaminio." Wasioamini hata hawamo, unaona. Wewe ni wa kuhurumiwa tu. Kuna kasoro mahali fulani. Kwa hiyo kama wewe ni mwaminio, mbona, ni kwa ajili yako. Kama wewe si mwaminio, basi si kwa ajili yako.

Ndipo mtu fulani akasema, "Waweza. . .?" Nilikuwa huko nje mtaani siku moja, kasema, "Waweza kumwambia mtu huyu anayesimama pembeni ana shida gani?"

17 Nikasema, "Unajua, Mungu huchukua mtu Wake bali kamwe si Roho Yake." Roho Yake juu ya Eliya ilikuja juu ya Elisha, kisha juu ya Yohana. Ile iliyokuwa juu ya Yesu ilikuja juu ya Kanisa, na kuendelea hivyo kote katika wakati. Shetani hufanya jambo lile lile. Yeye humchukua mtu wake bali kamwe sio roho yake. Nikasema, "Karibu ninakumbushwa hapo walipofunga kitambaa machoni mwa Yesu kule mahakamani asubuhi ile, wakampiga kichwani kwa tete, na kusema, 'Tabiri utwambie ni nani aliyekupiga nasi tutakuamini.' Kamwe hakufungua kinywa Chake na kusema Neno, kwa sababu hakuwafanyia watu vitimbi; Yeye alimtii tu Mungu." Mnaona?

18 Shetani alimwambia "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, mbona, fanya mwujiza hapa mbele zangu. Hebu niuone." Mmesikia hilo likisemwa. Mnaona? Kumbukeni tu, huyo ni ibilisi. Mnaona? Huyo ndiye. Mnaona? Yeye alisema, "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu," kasema, "fanya—fanya tu mwujiza na kuugeuza mkate huu. . .jiwe hili—hili liwe mkate nami nitakuamini."

Akasema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate pekee.'"

Na halafu pale msalabani, Shetani na wale makuhani walisema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka utoke msalabani. Ndipo tutakuamini."

19 Angeweza kufanya hivyo, bali angekuwa akimtii Shetani. Unaona? Yeye hafanyi yale asemayo Shetani; hufanya yale asemayo Mungu. Na mtumishi yeyote wa Mungu hufanya vile vile, kutii tu. Kwa hiyo unaposikia matamshi hayo, kumbuka tu mahali yanapotoka.

20 Usi—usiwadharau watu, bali wahurumie kwamba wamo katika giza kuu na upofu, labda wamekusudiwa hukumu hiyo. Kisha nini? Hilo ni baya, sivyo? Hmm? Kwa hiyo tunasikitika tu na kuendelea, kuwa wanyenyekevu, na kuwa Wakristo.

21 Sasa, usiku wa leo ninataka kuwazungumzia juu ya somo dogo ambalo labda. . .kidogo tu kuninii, mpaka tutakapolifanya kusanyiko letu kidogo kuwiana, na kuanza kuacha ushirikina wote ufutiliwe mbali.

22 Basi jana jioni nilifikiri kwa mara ya kwanza ilikuwa ni vizuri sana kuwaona wengi wakimwitikia Roho Mtakatifu. Hakika ningeweza kuhesabu angalau kumi na wawili papa *hapa* ndani ambao walidhani ilikuwa ni mzaha ama kitu kama

hicho, lakini mtakuwa na hayo kwa vyovyote vile, mwajua. Kwa hiyo kamwe msiruhusu hilo liingilie wale wanaoamini. Hao ni wasioamini, makafiri, na katika hali mbaya. A-ha. Basi waombeeni tu.

Lakini sasa usiku wa leo, ninataka kuliendea somo la *Makongamano*.

Sasa, ninataka kusoma Andiko linalopatikana katika Isaya 1:18:

> *Haya, njoni. . .tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa. . .nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa* nyeupe kama *sufu*.

23 Hicho ni kifungu kinachojulikana sana cha Injili. Labda wachungaji wenu wamekiendea mara nyingi. Nami nafikiri ni kimoja cha vifungu maarufu sana, ama vyenye huruma, vya Agano la Kale: Mungu akijaribu kufanya kongamano pamoja na watu kuhojiana mambo. Yehova Mungu, Yeye aliyeumba mbingu na nchi na viumbe vyote vilivyomo, na hata hivyo angeomba kufanya kongamano na watu kusudi, "tusemezane, tuone vile ingekuwa."

24 Tunasikia mengi sana siku hizi juu ya makongamano. Kumekuwako na mengi sana ya hayo, na kuna makongamano mengi sana yanayofanywa kote nchini, kote ulimwenguni. Nilikuwa huko Visalia, Illinois, majuma machache yaliyopita, ama Visalia, California, majuma machache yaliyopita, nasi tulikuwa kwenye jengo la ghala la silaha, kitu kama hili ama kubwa kidogo.

25 Basi alasiri ya kwanza kulikuwako na watu wengi waliosongamana ndani yake, kabla giza halijaingia walikuwa wamewafukuza karibu mamia mengi. Ndipo usiku uliofuata kulikuwako na karibu elfu mbili, kwa hiyo tusingeweza kukaa kule zaidi. Tulienda kwenye uwanja wa maonyesho wa mji jirani. Kufikia saa tisa alasiri hiyo kulikuwako na wengi sana mle, iliwabidi kufunga malango na kutowaruhusu kuingia baada ya saa tisa alasiri, kwa hiyo, kusongamana tu wakiingia.

26 Nao wanajiandaa sasa kujenga jengo kuu kwenye mji mwingine jirani kwa ajili ya kusanyiko kubwa, jumba kuu la mikutano la manispaa. Nami ninasahau itagharimu milioni ngapi za dola, nyingi sana ningesema, labda, dola milioni ishirini na tano, thelathini. Nao walisema, ama, walilitangaza kwenye redio na kwenye magazeti, ya kwamba katika muda wa miaka miwili wangelipia hata na zaidi jengo hilo kwa makongamano pekee. Na kwa kuwa walikuwa wakitaka kupapata mahali hapa pakuu, ambapo vilabu vingi vikuu na kadhalika, ambavyo hufanya makongamano yao, na vyama na kadhalika, vilikuwa. . .tayari walikuwa wakijaribu kujiwekea nafasi kwa miaka kadhaa awali, ikiuletea huo mji pesa, za

watu wanaoingia mjini kwa ajili ya makongamano haya na—na mikutano na kadhalika.

27 Tunaona ya kwamba kuna kukusanyika kwingi sana katika siku hizi za mwisho, zaidi ya ilivyokuwa. Nami nafikiri wakati umewadia kwa ajili ya watu wa Mungu kuanza kukutana zaidi. Hmm. "Haya njoni, tusemezane," asema Mungu, mnaona.

28 Nafikiri wakati umewadia kwa makanisa kuja pamoja, tofauti zetu ziraruliwe mbali, na ninii zetu. . .tukusanyike pamoja tukiwa mmoja. Yesu aliomba ya kwamba tupate kuwa mmoja: ". . .hivi watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana, mmoja kwa mwingine." Nao wakati umewadia, nafikiri, katika wakati huu, kwamba inatupasa kuwa tukikusanyika pamoja na kuwa mmoja zaidi, kwa kuwa hatujagawanyika. Tunayo mawazo tofauti, kama tu vile alama zetu za vidole gumba zisivyofanana, na—na shauku zetu za chakula, labda, hazingekuwa sawa; lakini hata hivyo, kimsingi sisi ni wanadamu. Na hivyo ndivyo ilivyo katika Ukristo: tofauti zetu za madhehebu yetu, hata hivyo tu mmoja. Sisi ni mmoja kwa kuwa tu watoto wa Mungu, waliozaliwa kwa Roho Wake, tukaoshwa katika Damu Yake.

29 Na hiyo ndiyo sababu tuko hapa usiku wa leo, ni katika kongamano. Haya ni makongamano ambamo sisi hukusanyika. Tumekuwa nayo nchini, kitaifa. Hapa katika Vita vya mwisho vya Dunia, wengi wenu watu wa rika yangu na wenye umri mdogo zaidi wanaweza kukumbuka Vi—Vita vya Pili vya Dunia, wakati walipokuwa na makongamano.

30 Tunashangaa makongamano ni kitu gani. . .ni ya nini, hata hivyo? Ni kwa ajili, ili wao wapate kuchukua kundi le—lenye akili kuliko yote na kukusanyika na kujaribu kupata mbinu za kufanya jambo fulani. Yanafanywa kwa kawaida wakati wa hali ya hatari, ndipo wanapofanyiza makongamano pamoja, wakati wa hali ya hatari. Ingekuwa ni wakati mzuri sana kufanya moja katika kanisa la dunia nzima la Mungu aliye hai, sivyo, kwa sababu ya hali ya hatari inayotukabili: ukomunisti na—na mambo yote, itikadi za ulimwengu. Kanisa linapoa. Basi ni wakati wa sisi kuja pamoja na kusemezana, kupatana juu ya mambo haya.

31 Sasa, waliliita moja ya makongamano, ya makongamano ya ulimwengu, Wakuu Wanne. Wengi wenu mnakumbuka hilo, wakati zile milki za Wakuu Wanne zilipokutana. Mpendwa wetu mwenyewe Dwight Eisenhower, rais wetu, na halafu pia Churchill, na hizo milki zingine kuu za ulimwengu, zilipofanyiza lile Kongamano la Wakuu Wanne. Kulikuwako na hali ya hatari. Mataifa yalikuwa. . .hili. . .mataifa yanayopenda amani yalikuwa katika wakati wa hatari, wakati Hitler na Nazi na. . . zote zilikuwa karibu kuuangamiza u—ulimwengu. Nao watu wapenda amani, wanaomcha Mungu, na urithi wetu mkuu,

ulikuwa hatarini. Kwa hiyo walikuja pamoja kwa ajili ya kongamano.

32 Kulikuwako na Kongamano la Geneva. Sote tunaweza kukumbuka Kongamano la Geneva, na pia Kongamanno la Paris, na jinsi ambavyo wanafanya hivyo. Wanaona ya kwamba kuna hali ya hatari inayoibuka, ndipo wanawaita walio bora kuliko wote wajuao. Viongozi wa mataifa wanakusanyika na kusemezana wao kwa wao yale watakayofanya. Wanachagua mahali fulani na. . . mahali ambapo panavutia.

33 Ndipo wanafika mahali hapa na kuzungumza na kuweka maoni yao pamoja, jinsi ambavyo wanaweza kuja pamoja kama kiongozi mmoja mkuu, kama taifa moja kuu, kama jeshi moja kuu, wote wakiungana kuwa mmoja.

34 Hiyo ingekuwa ni vile. . . Tungefanya jambo kuu kama kanisa lote lililokombolewa la Mungu lingeungana pamoja na kufanya jambo lile lile. Sote tuweke chini mawazo yetu madogo na maskini tofauti ambazo—ambazo huwatenganisha watu, nasi tungeweza kuja pamoja kama umoja mkuu wa Mungu. Ukomunisti ungetimua mbio; ninii. . . itikadi zingine zote zingetoroka, wakati jeshi kuu la Mungu likipata kuja pamoja.

35 Sasa, tunaona ya kwamba katika sehemu hizi za kukutania wanajaribu kupata mahali ambapo panavutia. Nilikuwa. . . Nimekuwa Geneva ambako walifanyia Kongamano la Geneva. Hakika ni mahali panapovutia. Kuna kitu fulani kuhusu mahali ulipo, hali zinazokuzunguka zinazoumba mazingira, panakusaidia sana.

36 Ninaweza kuwazia juu ya nyakati kuu sana za maisha yangu (mimi ni mtu anayependa mambo ya nje.) ni kwenda huko nje milimani na kuangalia kutua kwa jua, kusikiliza mlio wa wanyama mwitu, kuwasikia ndege. Kunavutia; ni kitu ambacho kinakufanyia jambo fulani.

37 Ndipo tungeweza kuja mahali ambapo tunaweza kuvutiwa kwa kuja pamoja, mahali pa kukutania. Baadhi yetu tungekuwa baridi na tofauti kidogo, kutokuhudhuria mkutano wa maombi Jumatano usiku, kukaa nyumbani kutazama kipindi fulani cha televisheni kisichopaswa kuwapo. Nao watu wanapumbazwa na hicho na kutohudhuria mkutano wa maombi, wapate kutazama kipindi fulani cha kishenzi.

38 Basi tunapokusanyika katika uamsho huu ni kuleta karama zetu na huduma yetu pamoja, kuzileta pamoja kwa ajili ya uamsho tupate kuleta uvuvio juu ya watu: kukusanyika pamoja kwa ajili ya kuzuka kwa uamsho, ama, sasa, kwenda nyumbani kwa Kanisa, kwa kuwa tuko karibu na wakati wa mwisho.

39 Hilo linajulikana dhahiri, kwamba tuko karibu na mwisho. Na sasa, kama tulivyoihisi mikutano, siku moja ama mbili

usiku tunapoendelea, tuone ni njia ipi Roho Mtakatifu atakuwa akituelekeza, tutalifikia, Bwana akipenda.

40 Lakini sasa, uvutio, ni mahali na mazingira unayoweza kuingia ndani yake, lakini kuvutiwa. Mimi, nikiwa ni mpenda mambo ya huko nje, ninapenda kupanda milimani na kusikiliza mlio wa wanyama pori. Nami nimekupenda tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Sio zaidi sana kuwinda mnyama, bali kuwa tu mwituni, kwa kuwa kuna kitu fulani kinachovuvia kwangu.

41 Hapa miaka michache iliyopita nilikuwa hapa juu Colorado, ambako mimi ni kiongozi kwenye misafara; nimekuwa nikiwapeleka watu huko nje kwa miaka kadhaa. Siku moja mimi na mfugaji tulirudi tumechelewa, baada ya wengi wa... sisi...inaitwa "ranchi za utalii", walikuwa wameingia na kupata paa wao na kadhalika, kisha wakatoka. Ndipo tukarudi, huko juu sana mlimani. Na huko ndiko ninakokuwa na kongamano dogo la kibinafsi, kila wakati ninapopanda kule juu, pamoja na Bwana. Daima Yeye hunionyesha jambo fulani, ama kunivuta karibu Naye, wakati ninapojitenga na kila kitu.

42 Basi mwaka huu theluji ilikuwa imechelewa kidogo nalo kundi la kulungu lilikuwa huko juu. Kulikuwako na theluji huko juu, kwa hiyo ilinibidi kupanda juu zaidi kuwapata kulungu. Alasiri moja huko juu, ilikuwa yapata Oktoba iliyopita, ma—majani yatetemekayo, huko chini, yalikuwa tu kama mienge, yamekauka na ni mepesi sana kuvunjika. Nami nilikuwa huko juu kwenye theluji. Nayo hali ya hewa inaweza kubadilika upesi sana kule juu. Dakika moja inaweza kuwa ikinyesha, kisha theluji inaingia, halafu jua linawaka. Ndipo dhoruba ikatokea, nami nikaenda nyuma ya mti na kuilaza chini bunduki yangu na kungojea mpaka huo mvumo ulipokwisha.

43 Nami nilikuwa papo hapo karibu na maskini mwanya mmoja karibu na mpaka wa msitu. Hapo ni kadiri misitu inavyokua, mpaka unafikia kwenye misonobari mbilikimo, na kadhalika. Ndipo niliposhangaa jinsi...Nilikuwa nimeketi hapo nyuma ya mti, nikisikiliza upepo ukivuma, na kuwazia juu ya Bwana, nyuma ya msonobari mkubwa. Ndipo baada ya kitambo kidogo dhoruba ikapungua. Nikasimama, nikaangalia pande zote.

44 Nalo lile kundi kubwa la kulungu nililokuwa nikijaribu kulifikia, lilikuwa limetenganishwa wakati wa hiyo dhoruba, nami ningeweza kuwasikia hao dume wakubwa wakilia. Loo, kuna kitu fulani kulihusu ambacho kinatia kitu kilicho hai ndani yako, kuwasikia jamaa hao wakilia; ninawaheshimu sana. Kisha huko juu mlimani nikamsikia mbwa mwitu akilia, mwenzake akijibu huko chini. Nikaangalia magharibi nalo jua lilikuwa likitua, na kama tu kupenya kwenye mianya ya milima, jicho kubwa la kiajabu sana, ilivyoonekana, la Mungu kuangalia kote juu ya mlima, upeo wa samawati; na kuona basi ambapo upepo ulikuwa umevumia na ma—maji yalikuwa yameganda juu ya

mimea isiyokauka ndipo ikafanya upinde wa mvua ulioenda kote ng'ambo ya lile genge.

45 Loo, yote hayo kwa jumla, nilivurugika tu kama mtoto mchanga nikaangua kilio. Huyo hapo, Mungu katika upinde wa mvua, lile agano; alionekana kama Alfa na Omega, yaspi na akiki, Rubeni na Benyamini pia, wa kwanza na wa mwisho. Huyo hapo, akilia pale katika yule mbwa mwitu; huyu hapa, akilia katika—katika yule kulungu. Kila mahali unapoangalia huko juu, palionekana kuwa ni Mungu.

46 Hivyo ndivyo ninavyopenda kupata huo uvuvio. Kupanda kule juu peke yangu pamoja na Mungu, juu kabisa. Maili na maili na maili, nisingeweza kushuka chini kwa siku kadhaa, kuninii. . .nilizohitaji kushuka kutoka mahali nilipokuwa kufika mahali farasi walipokuwa wamefungiwa. Lakini kule juu tu peke yangu na Mungu. Kulala huko nje usiku huo mlimani.

47 Na wakati tulipokuwa huko juu nilipata moja ya hizo roho za shangwe halisi juu yangu. Nadhani sio kitu cha kigeni kwenu Wapentekoste. Ndipo nikawa na furaha sana nikailaza bunduki chini kuegemea huo mti kisha nikaanza kukimbia kuuzunguka huo mti, nikirukaruka tu huku na huku kwa nguvu nilivyoweza nikipiga makelele kwa sauti yangu yote, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!" Nami nadhani kama mtu angekuja mwituni, wangaliwazia kulikuwako na mtu fulani ameitoroka hospitali ya wendawazimu.

48 Nikazunguka na kuzunguka mti huo, kwa nguvu tu nilivyoweza, nikipiga makelele na kuipiga mateke miiba ya misonobari. Ilinibidi kutoa mvuke mahali fulani la sivyo ningalipasuka. Ilikuwa ni ninii tu, nilikuwa tu nikiwa na wakati mzuri sana, maana nilikuwa moja kwa moja Mbele za Mungu, nikifanya kongamano pamoja Naye, nikizungumza tu, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu!

49 "Wewe hapo, kila mahali. Uko huko angani, kwenye jicho la kiajabu la jua, likiangalia huku na huku kote duniani. Wewe Huyo hapo katika upinde wa mvua. Wewe Huyo hapo ndani ya mbwa mwitu. Wewe Huyo hapo katika kulungu. Wewe Huyo hapo katika upepo; kuzisikia zikivuma kupitia kwenye hiyo misonobari kana kwamba kusema, 'Adamu, uko wapi?'" Unaona, nikienda pande zote, uvuvio, kongamano halisi na la kweli, nikilifanya na Mungu.

50 Ndipo mara nikakatizwa. Wala si—sipendi kukatizwa katika nyakati kama hizo, kwa hiyo, ninapenda tu kupaza sauti mpaka ni—nitosheke kabisa. Ndipo nikaangalia huko juu na kulikuwako na maskini kuchakulo mdogo wa misonobari. Loo, yeye ni maskini mhuni mdogo, yapata urefu *huu*; ndiye polisi mwenye koti la bluu wa mwituni. Naye ataogopesha kila kitu nchini. Nao wote humsikiliza, kwa kuwa sikuzote yuko tayari

"kwee, kwee," kupayukia kitu fulani. Akaruka juu ya kisiki cha kale ama gogo kule, akaniangalia na kuanza kubweka kwa nguvu tu alivyoweza, "Kwee, kwee, kwee, kwee."

51 Nami nikawazia, "Vema, kwani jamaa huyu mdogo ana shida gani." Nikasema, "Kwani hupendi hilo?" Nikasema, "Hebu angalia hili, basi." Ndipo nikazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka na kuzunguka huo mti tena. Naye akaendelea tu kupayuka zaidi. Nikasema, "Mimi ninamsifu Muumba wangu, ewe jamaa mdogo." Nikasema, "Nina wakati mzuri pamoja Naye. Tunafanya kongamano hapa. Nilimwambia ya kwamba nilikuwa mtupu na Yeye ananijaza, unaona? Hivi ndivyo mambo yaendavyo." Basi nikazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka huo mti tena.

52 Ndipo ikatokea nikaona maskini jamaa huyo hakuwa akiniangalia sana, kwa kuwa aliendelea kukigeuza maskini kichwa chake upande, maskini jicho lake limetokeza shavuni, karibu limetokeza, akiangalia chini namna *hii*. Vema, nikasimama, nami nikawazia, "Sasa ni kitu gani kinachonikatiza?" Ndipo nikaangalia chini kwenye huo mwanya. Kumbe kwenye wakati wa dhoruba tai mkubwa alikuwa amelazimika kushuka ki—kichakani ambapo miti ilikuwa imeshikana na miaka kadhaa hapo kabla ilikuwa imeshushwa chini. Naye alikuwa akimlilia ama—ama kumgombanisha tai huyu, naye huyo tai mkubwa alikuwa akitambaa kutoka chini ya kichaka hiki. Ndipo akaniangalia, na kuruka juu ya lile gogo.

53 Nami nikawazia, "Vema, sasa, kuna nini cha kiungu sana kukuhusu wewe?" Nami nikamwangalia namna *hiyo*, nami nikawazia, "Vema, Mungu, kwa nini ukaniacha nikome kukuabudu Wewe na kupaza sauti, kumtazama tu maskini yule tai?" Vema, tai. . .Mungu hujifananisha Mwenyewe na tai, na Yeye huwaita manabii Wake "tai" kwa sababu tai anaweza kuruka juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote aliyepo. Hakuna kitu kinachoweza kumfuata. Kama koho angejaribu kumfuata, angevunjika-vunjika hewani. Na hiyo ni kweli.

54 Yeye ni. . .vema, yeye ana jicho hata anaweza kuona akiisha kufika kule juu. Hiyo ndiyo sababu ninasema, mtu yeyote anayeruka juu, ruka tu juu kadiri unavyoweza kuishi, wajua. Hivyo tu, kwa sababu inafaa nini kwako kupanda juu, endapo huwezi kuona kitu wakati ukiwa huko juu? Haifai kitu. Kwa hiyo yeye—yeye anapanda kule juu, naye yuna jicho hata anaweza kuona vitu vilivyo mbali sana kabla havijafika huku, na hiyo ndiyo sababu Mungu aliwafananisha tai na manabii Wake, ama, manabii Wake na tai; na Yeye akajiita Mwenyewe "Yehova-Tai," kwa hiyo. . .nasi ni "wanatai."

55 Sasa, kuna tofauti kubwa kati ya tai na kuku. Wote wawili ni ndege, bali mmoja wao ni wa ardhini na huyo nwingine

ni wa mbinguni. Kwa hiyo hiyo ni tofauti kubwa sana, ila tu wao ni kama binamu ama kitu fulani. Kwa hiyo kama kuku hawezi kuiondoa miguu yake ardhini, usijali; yeye ni kuku tu kwanza, wajua. Kamwe hatafika kule juu na kujua yale tai ajuayo, ambaye anaweza kuruka huko mbinguni.

56 Kwa hiyo nilimwangalia jamaa huyu wakati akiketi pale, na macho yake makubwa mno ya kijivu akiniangalia. Nami ni—nikawaza, "Vema, kuna jambo moja ninalopenda kumhusu. Haogopi." Nami na—nachukia mwoga, vivyo hivyo, Mungu pia. Kwa hiyo, mtu anayeogopa baada ya kuponywa kushuhudia hilo, mtu ambaye Mungu amemwokoa kisha anaona aibu kumwambia mtu fulani ya kwamba ameokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu, sina matumaini makubwa katika wokovu wake. Kwa hiyo, wakati unapoupata kweli unataka kumwambia kila mtu. Kamwe huwezi kutulia. Kile kanisa linachohitaji ni Roho Mtakatifu zaidi na Moto ndani yake unaoliendesha; unaoliendesha kanisa. Inahitaji moto kuliendesha kanisa.

57 Kwa hiyo maskini jamaa huyu, nilimwangalia kwa dakika chache, na baada ya kitambo kidogo, akiisha kuona ya kwamba nilikuwa nikipendezwa naye, nikamwambia, "Hei, unajua ningeweza kukupiga risasi kabla hujaondoka kwenye gogo hilo?" kuona tu, kuona tu kama alikuwa akiniogopa. Hakuogopa, aliketi tu pale. Ndipo nikaona . . . "Ni kitu gani kinachokufanya ujiamini sana hivi?" Niliona aliendelea kuyasongesha mabawa yake, akihisi tu kama manyoya yote yalikuwa katika hali nzuri. Maana alikuwa na matumaini makubwa katika mabawa hayo, naye alijua ya kwamba angekuwa ameingia humo msituni kabla sijaweza kuigusa bunduki hiyo. Basi hapo nikapata somo. Nikawazia, "Hapa katika kongamano hili ninajifunza jambo fulani," mnaona.

58 Sasa, huyo tai alikuwa na mabawa mawili ambayo Mungu alimpa, naye alikuwa na matumaini katika mabawa hayo. Alijua yale angaliweza kufanya na mabawa hayo, wala hakuniogopa hata kidogo. Kwa hiyo alijua angeweza kuingia katika msitu huo kabla hata sijaweka mkono wangu juu ya hiyo bunduki.

59 Nami nikawazia, "Kama tai huyo, akiwa—akiwa na mabawa mawili aliyopewa na Mungu, alijua ya kwamba angeweza kutoroka kabla sijaweza kufanya lolote kulihusu, Mkristo aliyempokea Roho Mtakatifu anapaswa kufanya nini . . .?" Mradi tu unaweza kuhisi Uwepo Wake karibu nawe na kila kitu kinaenda katika utaratibu ("Hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wanaoenenda si kwa kufuata mambo ya mwili, bali ya Roho."), unapohisi hali hiyo ya kukimbia, usi—usiogope yale Shetani atakayofanya. Ninii tu, unajua uko katika uhusiano mwema basi.

60 Kwa hiyo nikamwangalia namna hiyo. Ndipo nikatambua, yeye hakuniogopa, bali hakutaka tu kusikia kuchakulo huyo

wa ardhini, maskini kuchakulo wa misonobari, ameketi hapo akifanya "Kwee, kwee, kwee. Kwee, kwee, kwee," kana kwamba atamrarua vipandevipande; mbona, hakuwa anaenda kufanya kitu, alikuwa ni mdogo mno. Huyo tai angaliweza kumnyanyua juu na hiyo ingalikuwa...mbona, mguu wake ulikuwa ni mkubwa kuliko huyo kuchakulo. Kwa hiyo, bali maskini huyo kuchakulo alikuwa akiruka juu chini kana kwamba atamrarua vipande-vipande, akijifanya tu, mwajua.

61 Hatimaye maskini huyo tai akachoshwa nalo. Kwa hiyo alifanya tu mruko mmoja mkubwa, akapigapiga mabawa yake kama mara mbili, kisha akaweka mabawa yake sawa. Nami nikasimama pale na kumwangalia tai huyo hata nikalia. Kamwe hakupigapiga mabawa yake, pop, pop, pop. Alipigapiga mara chache tu mpaka akafikisha ninii yake...juu ya mpaka wa ule msitu, halafu basi alijua tu jinsi ya kuweka mabawa yake kwenye hayo mawimbi ya hewa yaliyopanda kutoka mlimani; nayo yakambeba tu na kuendelea, mbele, mbele, mpaka akawa tu ni doa dogo. Wala hakusogeza unyoya, yeye alijua tu la kufanya.

62 Ndipo nikawaza, "Hivyo si ndivyo ilivyo? Sio, jiunge na Methodisti, kisha uende ukajiunge na Wabaptisti, kisha ujiunge na Waassemblies, na halafu ujiunge na Church of God. Sio pop, pop, hapa; na pop, pop, pale; ni kujua tu jinsi ya kuweka mabawa yako ya imani katika nguvu za Mungu, ndipo wakati utukufu unapoingia, uendeshe tu juu yake, mbele, mbele."

63 Viondokee maskini hivyo vijikuchakulo vya ardhini, vinavyosema, "Kwee, kwee, siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, hakuna Roho Mtakatifu tena. Ilikuwa ni kwa ajili ya mitume muda mrefu uliopita." Weka tu mabaya yako na uruke uende, mbele, mbele, mbele, mbele, mpaka huwezi kusikia hayo tena. Hiyo ndiyo aina ya kongamano tunalotaka pamoja na Mungu, litakalotuinua juu ya vivuli, litakalotupeleka mbali hata ukosoaji wote na chochote kile, huwezi kuusikia tena, umefungiwa tu ndani pamoja na Mungu. Haikubidi kujiunga na hili, kujiunga na lile. Jua tu jinsi ya kuweka imani yako.

64 Hiyo ni kweli. Iweke tu imani yako katika Neno la Mungu. Ndipo wakati Agano hilo la Kale na Jipya litakapotandazwa pale ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na hapo nguvu za Mungu zitakapoingia, ingia pamoja nazo. Panda tu juu, juu, juu, juu, juu, kote kote. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hawezi kushindwa.

65 Loo, makongamano haya, inapaswa kuwa ni kuzingatia kwa njia ya maombi kwetu sisi sote. Haitupasi kuacha tu moja lifanyike pasipo kuliombea, kimataifa na kikanisa pia na chochote kile. Inatupasa kuomba sikuzote.

66 Rafiki yangu mhudumu, ndugu mzuri Mkristo, kwenye. . . wakati wa Kongamano la Geneva, alikuwa akiingojea redio yake, kusikiliza taarifa yake rasmi, kwa sababu taifa letu lilikuwa hatarini, nao urithi wetu mkuu ambao babu zetu waliupigania ulikuwa hatarini. Naye alikuwa ni mtu mwema, mzuri mwenye haki. Alikuwa ameketi akisikiliza.

67 Mtu fulani akabisha mlangoni pake. . .mhuni mamboleo, akiwa na ndevu zake, mchafu. Inawezekanaje kwamba watoto wa Kimarekani waendee upuuzi kama huo, kisha watoke huko nje. . .Akabisha mlangoni, naye akasema, “Bwana, nipo hapa kuuza mashairi yangu na nyimbo zangu,” akasema, “wala hawatanisikia.” Kisha kasema, “Hawatanisikiliza. Nao wananiambia wewe ni mtu aliyeshawishiwa. . .mtu mwenye ushawishi mjini.”

68 Akasema, “Mtu mwema, ingia uketi chini kwa dakika moja tu. Ninasikiliza taarifa maalum.” Lakini, loo, asingeweza kusimama kimya. La, bwana. Yeye. . .labda. . .hiyo ilikuwa ni muhimu sana kuliko taarifa ya taifa.

69 Na hivyo ndivyo wengi sana wa wafuasi wa kanisa wanavyofanya siku hizi, mambo hayo madogo ya kijinga yanayotukia miongoni mwa watu ni muhimu kuliko Kanisa halisi la Mungu aliye hai. Hebu na tusahau mambo yetu madogo na turuke twende. Hebu tusikilize taarifa rasmi.

70 Sasa, hapa si. . .walikuwa na kongamano lingine ningetaka kulizungumzia kwa dakika moja tu: kongamano la mwisho walilofanya kwenye jengo la U.N., ambapo Magharibi na Mashariki zilikutana, ambapo Khrushchev alitoa kiatu chake na kulipiga dawati kwacho. Eisenhower na Khrushchev walikutana, Eisenhower akiwakilisha ule ulimwengu tano huru naye Khrushchev ulimwengu wa Komunisti ya Mashariki. Nalo hilo halikutambulikana na watu wengi, hawakuliombea.

71 Lakini kama ilitokea uliona ya kwamba hilo lilikuwa ni jibu la moja kwa moja na unabii wa moja kwa moja ukitimizwa wakati huo. Ulikuwa ni unabii wa moja kwa moja. Mashariki na Magharibi zilikuwa zimetimiza vile hasa alivyosema Danieli, ya kwamba, pale, falme kumi, zingekuwako, zisingechanganyikana, kama vile chuma na udongo visingechanganyikana. Nalo Neno *Khrushchev* katika Urusi linamaanisha “udongo”; neno *Eisenhower* katika Kiingereza linamaanisha “chuma”; nazo chuma na udongo zisingeweza kupatana.

72 Loo, tunapoyaona mambo haya yakikaribia inatupasa kuwa magotini mwetu tukilia, “Ee Bwana Yesu, tufanyie jambo fulani mara moja.” Huenda tukajaribu kumvuta mtu wa mwisho ambaye anaweza kuingizwa katika Ufalme wa Mungu; kujikusanya pamoja na kufanya makongamano na mikutano na kukusanyika katika mikutano ya maombi usiku kucha. Shida ya

kanisa usiku wa leo, tunaenda tu na kupiga magoti, na kuomba na kupiga miayo mara chache, wenye kusinzia na wachovu, na inatulazimu kwenda nyumbani na kulala.

73 Sio kama kanisa la mwanzoni la Kipentekoste. Waliomba siku nzima na usiku kucha. Nilikutana na hawa watu wa zamani kutoka miaka arobaini iliyopita, wakasema waliomba siku nzima na usiku kucha, wakatembea mitaani. Siku hizi tumekuwa maarufu sana na tunataka kujilinganisha na makanisa makubwa, na hapo ndipo tunapofanya makosa yetu. Na—nawaambia, kanisa lilikuwa katika utaratibu bora zaidi miaka arobaini iliyopita kwa ajili ya Kuja kwa Bwana kuliko lilivyo usiku wa leo, kwa sababu sisi ni kanisa la Laodikia. Tunatambua ya kwamba huu ndio wakati tunaoishi. Nalo hilo lilikuwa ndilo kanisa pekee ambalo Yesu alipatikana nje ya kanisa Lake Mwenyewe akibisha mlangoni, akijaribu kurudi ndani ya kanisa Lake Mwenyewe.

74 Tofauti zetu zimemfukuza, utengano wetu wa udugu, na jinsi ambavyo tumeyafuatilia mambo ya ulimwengu badala ya mambo ya Mungu. Tunapaswa kuwa tumeingia kabisa kwenye nchi ya Kanaani, na sisi hawa hapa nyikani, tukizunguka-zunguka, na kuzunguka tena, kama tu vile wao walivyofanya kule nyuma. Tunapaswa kuwa na kila namna ya karama, ishara na maajabu makanisani mwetu. Badala ya hayo, Mungu anaweza akainua kitu fulani, halafu sisi sote tunakiogopa sana na kuondoka, na kusema hatuelewi mambo haya.

75 Unafikiri walifanya nini kwenye nyika hilo kwa muda wa miaka arobaini, wakitembea huku na huku, na kurudi kwenye maskini eneo lile lile? Tumechukua Matendo 2:4, Matendo 2:4, Matendo 2:4; tumerudia-rudia hata kufa. Hima twende mbele! Nchi ya ahadi ipo. “Kwa kuwa yoyote mtakayo, mkisali amininini mnayapokea nayo yatakuwa yenu.” Matendo 2:4 ni sahihi, bali hiyo siyo yote. Hiyo ni kweli. Kunayo mengi zaidi yake. Hiyo ni. . .kila ahadi katika Biblia ni yetu. Imetolewa kwetu na Bwana Yesu, na mkono Wake mkuu wenye nguvu unaushikilia wakati ili tuweze kuimiliki nchi ambayo tumepewa. Bila shaka.

76 Makongamano. Loo, wakati ulimwengu unapokuwa na kongamano nao wanakutana pamoja, wanafanya nini? Kwa kawaida hunywa wiski na kokteli, na kunywa, na kudanganya, na kusema uongo, na kudanganyana, wanafanya kila namna ya mipango mbalimbali na kadhalika, wakiwa na kisu nyuma yao, kama vile Biblia ilivyosema wangefanya.

77 Lakini inakuwaje wakati Mungu anapofanya kongamano? Watu hufunga na kuomba na kungojea maagizo, kisha wanasonga mbele. Tumekuwa tukizungumza sasa juu ya kongamano la ulimwengu, kongamano la taifa. Kunayo mengi tungeweza kuwazia, bali hebu tuwazie baadhi ya makongamano aliyokuwa nayo Mungu. Hebu tujikumbushe baadhi ya hayo.

78 Hebu tuwazie juu ya kongamano la kwanza ambalo Mungu alipata kufanya wakati hali ya hatari ya kwanza ilipotokea. Tutaliita "Kongamano la Edeni." Hiyo ilikuwa ndiyo hali ya hatari ya kwanza, wakati neno lilipofika Mbinguni ya kwamba mwana wa Mungu na binti Yake, watoto Wake aliowaweka katika Edeni, walikuwa wamepoteza mahali pao katika neema, nao walikuwa wamemwacha Mungu, na walikuwa wamerudi nyuma na wako uchi. Mbingu zisingeweza kumshikilia zaidi. Alishuka duniani, akitembea huku na huku katika bustani, akipaza sauti, "Adamu, Adamu, uko wapi?"

79 Mwanadamu alionyesha kweli kile alichofanyizwa kwacho papo hapo. Badala ya kumjia Mungu na kusema, "Nimekosea, Baba. Nimefanya makosa," yeye alijificha na kujifunika katika majani ya mtini. Hivyo ndivyo mwanadamu anavyojaribu kufanya siku hizi. Badala ya kutoka na kusema yeye ni asiyeamini, atajaribu kusema, "Mimi ni Mpresbiteri, Mbaptisti, Mmethodisti, Mlutheri," ama kitu kingine. Badala ya kujifunika katika haki ya Mungu, na kukiri dhambi zake kwamba amekosea na asiyeamini, yeye hujaribu kujificha nyuma ya thiolojia fulani ya kanisa. Toka nyuma yake, Adamu, ewe asiyeamini. Angalia, hivyo ndivyo yeye hufanya, hata hivyo.

80 Pia angalia, Mungu kamwe hakumtuma Malaika chini kumtafuta mtoto Wake; Yeye alikuja Mwenyewe. Hiyo ilikuwa ndiyo ninii halisi. . . Sababu nafikiri siku hizi, ya kwamba leo hii wakati wanapojaribu katika siku hizi za dini ya kisasa, siku hii wakati dini ya umma inaitawala nchi, ikinyemelea katika madhehebu yote mbalimbali. . . Wanajaribu kuondoa Uungu wote wa Yesu Kristo na kumfanya mwanadamu tu.

81 Sio muda mrefu uliopita nilikuwa nikizungumza na mwanamke fulani. Akasema, "Ninazithamini jumbe zako, Ndugu Branham, bali unaweka mkazo mwingi sana juu ya Yesu. Unamjivunia kupita kiasi."

Nikasema, "Kama ningalikuwa na ndimi milioni kumi, nisingeweza kumjivunia Yeye vya kutosha." Nikasema, "Yeye anastahili kila kitu ningaliweza kujivunia."

Akasema, "Vema, kunalo jambo moja: wewe unajaribu kumfanya Mungu."

Nikasema, "Yeye alikuwa Mungu."

"Loo," akasema, "yeye alikuwa ni mwanadamu tu. Alikuwa mtu mzuri."

82 Wao hawaamini katika Damu Yake ipatanishayo. Sikilizeni, kama hiyo ilikuwa ni damu ya Myahudi ama ya Mmataifa, sote tumepotea. Hiyo ilikuwa ni Damu ya Mungu Mwenyewe. Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa: Alikuwa ni Mungu aliyedhihiriswa katika mwili. Hiyo ni kweli kabisa.

83 Ni jambo gani lililotukia? Damu hutokana na jinsia ya kiume. Tunajua hilo. Kuku anaweza kutaga yai, lakini kama hajakuwa pamoja na ndege wa kiume, halitaanguliwa kamwe. Halijarutubishwa. Mtoto mchanga anazaliwa na mwanamke; amefunikwa katika damu yake, bali hana hata chembe moja ya damu ya mama. Himoglobini iko kwenye jinsia ya mwanamume. Kwa hiyo tunaweza . . .

84 Ni kama tu vile, msimu wa kuchipusha majani unakuja. Nasi tunaona maskini mama ndege wanatoka hapa nje na kujitengenezea kiota, wanataga kiota kizima cha mayai. Naye anaweza kuingia kwenye kiota hicho na kuyaatamia mayai hayo hata akonde sana asiweze kuruka kutoka kwenye hicho kiota, kwa uchaji sana, kwa heshima sana kwa mayai yake. Anayapindua *huku* na kuyapindua *kule*. Anakufa kwa njaa, bali anahofu ya kwamba ataninii . . . yataachwa wazi kama akiruka kutoka kwenye kiota. Yeye ni mama mwaminifu na anajaribu kuyaatamia mayai haya. Lakini endapo mume huyo . . . huyo ndege jike aliyeyataga hayo mayai, kama hajawa pamoja na ndege wa kiume, mwenziwe, hayo mayai, haidhuru atayaatamia jinsi gani, jinsi anavyoyatunza vizuri, yataozea moja kwa moja kwenye hicho kiota. Hiyo ni kweli kabisa.

85 Hiyo ndiyo shida ya mengi ya makanisa yetu ya kale, baridi, ya kawaida siku hizi, yana kiota kilichojaa mayai yaliyooza. Kitu pekee walicho, ni wenye kukiri, bali kamwe hawajapata kuwa na yule Mume, Yesu Kristo. Jambo pekee lipasalo kufanywa ni kulisafisha, na kuanza tena pamoja na wanaume na wanawake ambao wamekuwa katika uhusiano na yule Mume, Yesu Kristo kwa kanisa Lake.

86 Wanawezaje kuamini nguvu za kimbinguni za Mungu wakati hawana chochote cha kuaminia? Mama yangu mzee, wa Kusini, aliniambia, kasema, "Kipenzi, huwezi kupata damu kutoka kwa tanipu, kwa sababu hakuna damu ndani yake." Unawezaje kupata imani kutoka kwa mtu ambaye hana kitu cha kuaminia? Kama hujawahi kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, hujui kanuni ya kwanza ya nguvu za kufufuka kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Hawalielewi. Loo, tunazo. Nao ni watoa sadaka wakubwa kanisani, nasi tunawafanya mashemasi na kila kitu kingine, na kuwaatamia, nao ni wasioamini tu kwa kuanzia.

87 Sasa, jinsi hilo lilivyo kweli, kuona wakati wa kukaribiana. Yule Mwenzi . . . Sasa unapaswa kuwa ni wakati wa kukaribiana, wakati ka—kanisa linapoingia katika uhusiano na Kristo na kupata imani halisi ya kweli ya Roho Mtakatifu.

88 Basi mama huyu akaniambia, akasema, "Ndugu Branham, ulisema ulikuwa wa kimsingi; ulisema tu yale Maandiko yaliyosema na kudumu nayo."

Nikasema, "Naam."

Naye akasema, "Ninaweza kukuthibitishia ya kwamba Yeye hakuwa ni Mungu."

89 Nikasema, "Iwapo alikuwa chochote pungufu ya Mungu, Yeye alikuwa ndiye mdanganyifu mkubwa kuliko wote ulimwengu uliyepata kuwa naye." Nikasema, "Roho Mtakatifu, Mungu, alimtia uvuli bikira naye akaumba Seli ya Damu katika tumbo la uzazi. Seli hii ya Damu ilikuwa ni Mwana wa Mungu. Kupitia kwa Damu hiyo tunalo ondoleo la dhambi. Mwanadamu hakujua chochote kumhusu mwanamke huyo. Yeye alisema, 'Kamwe sikumjua mwanamume.' Naye huyo alikuwa ni Mungu Mwenyewe akifanya maskani pamoja na mwanadamu: Mungu, Mwenyewe."

Akasema, "Nawe ati unamfanya Mungu."

Nikasema, "Yeye alikuwa Mungu."

Akasema, "Nitalithibitisha kwa Biblia yako mwenyewe yeye hakuwa ni Mungu."

Nikasema, "Hebu nikusikie ukilisema."

90 Akasema, "Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, wakati Yesu alipokuwa akienda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema, 'Akalia.' Na iwapo alikuwa ni Mungu, hangeweza kulia."

91 "Loo," nikasema, "mama, hilo ni jepesi kuliko mchuzi uliofanyizwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa." Nikasema, "Ungewezaje kuwekea msingi thiolojia yoyote juu ya hilo?" Nikasema, "Yeye alikuwa Mwanadamu na Mungu pia."

92 "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote ila mwana pekee wa Baba amemfunua. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Kweli kabisa.

93 Nikasema, "Ilikuwa ni kweli, hapo aliposhuka kwenda kwenye kaburi la Lazaro Yeye alilia kama mwanadamu; bali wakati alipoyavuta maskini hayo mabega juu, akaangalia huko nje na kusema, 'Lazaro, njoo huku,' naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne akasimama kwa miguu yake na kuishi tena, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu akizungumza kupitia Mwana Wake. Kweli! Ilikuwa ni Mungu ndani Yake. Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati aliposhuka mlimani usiku huo akiwa na njaa, akitafuta chakula karibu na mti; Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati aliposhikwa na njaa, bali hapo alipozichukua zile biskuti tano na samaki wawili na kuwalisha watu elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu Yule aliyeweza kuumba. Sio samaki mwingine; bali samaki aliyepikwa, sio ngano zaidi; bali mkate uliookwa. Yeye alikuwa ni Mungu Muumba."

94 Alikuwa ni Mwanadamu amelala huko nje nyuma ya ninii. . .merikebu hiyo usiku huo wakati pepo waliapa watamzamisha. Labda pepo elfu kumi wa baharini walisema, "Tumempata amelala usingizi sasa nasi tunaweza kumzamisha."

Maskini merikebu hiyo ilirushwa-rushwa kama kifuniko cha chupa katika dhoruba huko nje. Wakawazia, "Tumempata sasa." Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokuwa amelala usingizi, amechoka na kudhoofika kutokana na ibada Yake, bali alipoweka mguu Wake juu ya demani ya hiyo merikebu, akaangalia juu na kusema, "Amani, tulia," nazo pepo pamoja na mawimbi zikamtii, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu.

95 Alipokufa msalabani, Yeye alilia kama mwanadamu. "Mungu Wangu, unirehemu. Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Yeye alikuwa ni Mwanadamu katika kufa Kwake; bali kwenye ile asubuhi ya Pasaka wakati alipouvunja muhuri wa mauti, kuzimu, na kaburi, na kufufuka tena . . .

96 Loo, imevuvia kila mshairi ama mwandishi wa nyimbo aliyewahi kuwapo. Mtu yeyote aliyepata kuwa chochote muhimu aliamini Yeye alikuwa ni Mungu. Iliwavuvia washairi na manabii kote katika miaka. Mmoja aliyeishi . . . mmoja aliandika shairi, kasema hivi:

> Niwonapo msalaba wa ajabu
> Ambapo Mfalme wa Utukufu alikufa,
> Ninahesabu umaarufu wangu wote kuwa ni hasara.

97 Eddie Perronet alisema:

> Wote lisifuni Jina la Yesu!
> Malaika na waanguke kifudifudi;
> Ileteni taji ya kifalme
> Mkamvike taji Bwana wa wote.

98 Mwingine, kipofu Fanny Crosby alisema:

> Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
> Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
> Unapowazuru wengine,
> Usinipite.
>
> Wewe Kijito cha raha yangu yote,
> Zaidi ya maisha kwangu,
> Ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe?
> Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?

99 Mwingine, Claire, aliandika hivi:

> Alipoishi, Yeye alinipenda; akifa, aliniokoa;
> Alipozikwa, aliondolea mbali dhambi zangu;
> Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
> Siku moja yuaja—loo siku yenye utukufu!

Mtu yeyote angeamini Yeye alikuwa ni Mungu. Bila shaka.

100 Loo, wakati Mungu alipokuwa na kongamano huko Edeni, mwanawe alikuwa amepotea, watoto Wake walikuwa wamepotea. Hiyo ndiyo sababu kamwe hakuuaminisha ukombozi kwa Malaika yeyote wala chochote kile ila Yeye

Mwenyewe. Tulikombolewa kwa Damu ya Mungu. Na sasa Seli hiyo ya Damu, hiyo ndiyo inayotupatia ujasiri wa kusimama juu ya Neno Lake. Hiyo ndiyo inayotupatia ujasiri wa kutembea machoni pa pepo na pingamizi, kwa sababu tunajua tunakuja tumefunikwa kwa Damu ya Bwana Yesu, ambayo ni nguvu za Kiungu katika Damu ya Yesu.

101 Sasa, mwangalieni Yeye. Tunaona kongamano hili, Mungu akipitia kwenye bustani ya Edeni. Kuna jambo linalopaswa kufanywa; kuna hali ya dharura inayoendelea. Watoto Wake wamepotea; hajui la kufanya. Anashuka katika bustani, anaanza kuwatafuta. Wakati alipowapata huko nyuma mle ndani, wamejificha nyuma ya kanuni fulani ya imani ya kujibunia, Yeye alifanya nini? Alichagua mti fulani na kuwaita watoke. Naye akafanya kongamano, na kulikuwa na uamuzi uliofanywa: jinsi ambavyo mwanadamu hana budi kukombolewa. Naye mwanadamu amefanya kazi juu ya majani ya mtini tangu wakati huo; bali Mungu kamwe hajatambua chochote ila damu aliyoanza nayo hapo mwanzo.

102 Kila mwanamume na mwanamke kote kupitia kwenye wakati, kila nabii, kila mtu, daima amepitia juu ya kanuni hizo. Ayubu alisimama imara juu yake. Mahali pa pekee pa kukutania pa Israeli palikuwa ni chini ya damu iliyomwagika. Mahali pekee Utukufu wa Shekina ulipoangukia palikuwa ni chini ya damu. Mahali pekee ambapo Utukufu wa Shekina utakuja. . . Msiniache niumize hisia zenu, Baptisti, Presbiteri. Lakini mahali pekee ambapo Utukufu wa Shekina huangukia ni chini ya Damu. Hiyo ndiyo sababu mnauhisi huu Utukufu wa Shekina wa Kipentekoste ni kwa sababu uko chini ya Damu, Damu iliyomwagika ya Mwana wa Mungu. Kurudi kwenye Utukufu wa Shekina, wakati alipoichukua Damu Yake Mwenyewe na kulipasua lile pazia mara mbili, nasi tunaingia kwenye Uwepo wa Mungu, Utukufu wa Shekina, ambamo baraka Zake. . . Loo, hufanya watu wapya kutoka kwa wa kale.

103 Haruni aliacha fimbo yake mle mwaka mmoja nayo ikachanua na kutoa maua wakati ikiwa katika uwepo wa Utukufu wa Shekina. Mtu yeyote anayekaa katika Uwepo wa Utukufu wa Shekina wa Mungu, atamchukua maskini mwenye dhambi aliyekufa, aliyekufa katika dhambi na makosa, na kumchanua akawa kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

104 Kongamano, kongamano, Mungu alifanya uamuzi Wake. Hilo ndilo tungeliita Kongamano la Edeni. Mnajua, wakati huu unapita upesi mno. Mnaona, hata hupati kuanza mpaka wewe. . . ni wakati wa kumalizia. Utukufu wa Shekina kwenye Kongamano la Edeni.

105 Sasa, kulikuwako na kongamano lingine. Hebu turejee kwenye mawili ama matatu zaidi upesi, mkipenda. Kulikuwako na kongamano lingine. Hebu tuliite "Kongamano la Kichaka

Kilichowaka Moto." Kulikuwako na mtu aliyetoroka wakati mmoja, nabii mtoro ambaye Mungu alikuwa naye. Akatoka akajiolea mke, kisha akawa na mvulana mdogo jina lake Gerishomu. Jina lake lilikuwa ni Musa. Kwa hiyo alikuwa anaenda kurithi kondoo wote wa Yethro, naye alikuwa akiendelea vizuri sana, wakati akiwa chini ya mlima asubuhi moja. Loo, alikuwa tayari amesahau mizigo ya watu huko chini Misri, kwa sababu alikuwa katika hali nzuri sana.

106 Nafikiri hivyo ni karibu vile kanisa la Kipentekoste limefikia, limesahau kuhusu mizigo ya hao wenye dhambi. Hiyo si kanisa la Kipentekoste pekee, bali la Methodisti, la Baptisti, la Presbiteri. Badala ya kuwarudisha kwa Mungu. . .Na mtu yeyote, sijali wewe ni mwanathiolojia gani, ama wewe ni mfuasi wa kanisa lipi. . .Kulikuwako na kanisa moja, na Ukristo wote ulianzia kwenye siku ya Pentekoste kwa tukio la Kipentekoste. Kanisa Katoliki lilisema hao walikuwa ndio. Kila mtu hujaribu kurejea nyuma kwenye hilo, lakini kama ilikuwa ni wao, kwa nini utukufu ule ule na ishara zile zile hazilifuati kanisa hilo lililokuwako wakati huo? Bila shaka.

107 Sasa, kulikuwako na kongamano. Mungu alimwona nabii Wake mtoro; na wakati Mungu anapomchagua mtu kufanya jambo fulani, hakuna njia kwake kuliondokea. Mungu humrudia mara kwa mara. Labda baadhi yenu hapa usiku wa leo, aliyerudi nyuma, utakuwa na mashaka siku zote za maisha yako (na unapaswa kuwa nayo) mpaka utakapojisalimisha kwa Mungu. Alikuwa ndiye huyo hapo.

108 Baadhi yenu wanawake, baadhi yenu wanaume, mnarudi huko nje ulimwenguni, mnaenda kwenye madansi na mambo ambayo mlifunzwa vizuri zaidi. Siku hizi ni aibu mahali makanisa yetu ya Kipentekoste yamefikia. Kama vile David duPlessis alivyosema siku moja, mahali tulipokuwa tumefikia. Mnajua sisi kanisa la Kipentekoste ni kama tu kanisa letu la Methodisti ambao tuko katika jengo lao usiku wa leo; kama kanisa la Baptisti, la Presbiteri. Kama Umethodisti ungeyarudia mafundisho ya John Wesley, ungekuwa ni sawa. Hakika. Kama Wabaptisti wangemrudia John Smith, Lutheri lingelirudi kwa Martin Luther, na iwapo Pentekoste ingerudi kwenye Pentekoste, hiyo ni kweli, ingekuwa ni sawa.

109 Lilianza vema, lakini jambo ni kwamba tunawaingiza wajukuu. Mungu hana wajukuu wowote. Yeye hana wajukuu wa kiume; Yeye anao wana tu. Tunawaingiza watoto wetu ndani na kuwaweka kwenye susu, kama vile Wamethodisti na Wabaptisti na wote hao. Wanakuja kanisani, nasi tunawapokea kama Pentekoste; wala hawajui zaidi kumhusu Mungu kuliko sungura ajuavyo kuhusu viatu vya theluji. Kile tunachohitaji leo hii ni kurudi kwenye ujuzi wa Mungu, na kurudi pamoja na Roho Mtakatifu tena. Hiyo ni kweli.

110 Sasa, samahani kwa tamshi hilo. Linasikika la kukufuru. Sikumaanisha kulisema tu jinsi hiyo. Bali hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Inatupasa kurudi kwenye. . .Mungu hana wajukuu. Yeye anao wana, bali sio wajukuu. Hakuna mahali katika Biblia ambapo Mungu alikuwa na mjukuu. Kila mtu hana budi kuja na kulipa gharama ile ile, hana budi kuja vile vile. Mungu anayo Njia moja tu, na hiyo ni Yesu, nawe huna budi kupitia Njia hiyo. Pasipo na hiyo, hakuna njia ya kumfikia.

111 Sasa, tunaona ya kwamba Musa aliridhika vizuri sana. Kila kitu kilikuwa kinaendelea vyema, naye alikuwa amepoteza mzigo wote kwa wale watu waliokuwa huko chini katika utumwa. Basi siku moja Mungu akaamua ya kwamba angemwita. Na kwa hiyo akachagua mahali, mti fulani.

112 Na mahali Mungu anaposhukia kuna, kwa njia moja ama nyingine, daima kuna Moto mwingi mahali alipo Mungu. Kama uko mahali alipo Mungu, kuna kelele nyingi na Moto mwingi. Sijui ni kwa nini, bali imekuwa hivyo daima. Hayo ni Maandiko. Naam, bwana, daima ni Moto mwingi. Na inahitaji Moto kulisogeza kanisa kwa vyovyote vile. Kamwe hutafanya jambo hilo. Kamwe hutawavalisha majani ya mtini. Kamwe hutawavalisha majani ya mtini ya Kipentekoste. Hawana budi kurudi kwenye ule Moto. Hiyo ni kweli.

113 Wakati mmoja mimi na ndugu yangu, tulipokuwa wavulana wadogo, tulikuwa tukitembea nasi tukamwona kasa. Tulidhani ndicho kiumbe cha kuchekesha sana nilichopata kuona, jinsi alivyoitupa-tupa hiyo miguu. Ninyi watu wa Illinois mnajua kasa ni nini. Naye huyu hapa akaja akitembea. Nikasema, "Si anaonekana wa kuchekesha, ndugu?" Tukasogea.

114 Inanikumbusha tu juu ya watu wengi, wakati ukiwakanyaga kwa injili, mwajua. Wanasema, "Shiiu," wanarudi kwenye ganda lao, mwajua. "Mimi ni *Fulani-wa-fulani*. Mimi ni mfuasi wa dhehebu hili." Hilo halina uhusiano wowote nalo. Hiyo ni kweli. "Mimi ni mfuasi wa *Hiki-na-hiki*." Vema, ningeona aibu kulikubali. Ninamaanisha huenda kukawa na msamaha kwake kama ukijaribu kwa bidii sana kutubu. Huenda ukasamehewa hilo.

115 Mungu hatambui dhehebu lolote. Yeye hutambua Damu ya Mwana Wake Mwenyewe, Yesu Kristo. Na hiyo ndiyo kila kitu. "Nitakapoiona hiyo Damu nitapita juu yenu." Naam.

116 Mimi na mvulana huyu tulikuwa huko nyuma, na maskini kasa huyu. Nikasema, "Unajua nitakachofanya, Mpenzi? Nitamfanya atoke hapo." Nikaenda nikajitafutia ufito na kumcharaza kwelikweli. Haikusaidia hata kidogo. Huwezi kuwaingiza ndani kwa kuwapiga. Ni hivyo tu. Kamwe huwezi kuwarejesha kwa kuwacharaza. Hiyo ni kweli. Nimekuwa nikijaribu hilo kwa muda wa miaka kumi wala siwezi kufanya hivyo. Kamwe huwezi kuwacharaza hata warudi kwake.

117 Kwa hiyo nikasema, "Nitakwambia yale nitakayofanya. Nitamshughulikia." Kulikuwako na kijito kilichopitia pale, kwa hiyo nikashuka na kumzamisha majini. Mapovu machache tu yakatokea na ni hayo tu. Ndugu, unaweza kuwabatiza kifudifudi, kichalichali, mara tatu, mara tano, wala haifai kitu; mapovu machache tu yatatokea na ni hayo tu yaliyosalia. Hiyo ni kweli. Ama, "Mungu abarikiwe, nilikwambia nitafanya hivyo," ushuhuda. Ni hayo tu kwa hilo.

118 Mnajua jinsi nilivyomfanya asogee hatimaye? Nilijitengenezea moto kidogo na kumwanika maskini jamaa huyo juu yake. Ndipo akaondoka. A-ha. Kile kanisa linachohitaji ni Moto mwingine wa Kipentekoste; Roho Mtakatifu hulifanya kanisa lirudi kwenye hatamu ya Mungu; kurudi kwenye hatamu.

119 Mungu hajali wewe ni wa dhehebu gani. Yeye anayapinga hayo yote hata hivyo, kwa hiyo wakati . . . Vema, hiyo ni kweli. Ninaweza kuthibitisha hilo kwa Maandiko. Katoliki ilikuwa ndiyo dhehebu la kwanza, ambalo lilikuwa ni kahaba na lilikuwa na mabinti. Sasa, unaweza kushika njia yako . . .

120 Mtu yeyote aliyewahi kusoma Baraza la Nikea, wazee Waliotangulia Nikea, chochote, utaona lilipofikia kwanza palikuwa ni kwenye Nikolai ambapo Mungu alichukia hilo tendo. Halafu muda si muda wajua likawa ni fundisho. Lilikuwa ni nini? *Niko* ni "kushinda"; *lai*, ni "ya walei": kuwashinda walei. Wanaweka utakatifu jukwaani na kuacha walei waulipie. Kwa hiyo haya basi. Kwa hiyo hilo ndilo hasa. Kwa hiyo sisi sote tunafuata hatua zile zile na kurudi moja kwa moja katika weusi tena upesi tu tuwezavyo kwenda.

121 Nilikuwa nikiwachunga ng'ombe. Nilisimama pale wakati mmoja. Shirika la Herefodi hulisha kwenye—kwenye Bonde la Troublesome River, na kama unaweza kuchangia tani moja ya nyasi kavu kwenye ranchi yako unaweza kuweka ng'ombe mmoja kwenye hayo malisho. Halafu basi, kadiri ya tani unazoweza kuchangia, hiyo ndiyo idadi ya ng'ombe ranchi ya— yako itakayotoa. Wanawatia alama na kuwaweka mle. Walikuwa na uzio wa kuzurura, wasije wakazurura kwenda kwenye mali ya wenyewe, wanaposhuka kutoka mlimani. Nilizoea kuketi pale pamoja na mwangalizi siku kadhaa, huku nimewekelea miguu yangu juu ya ncha ya tandiko, nikiwaangalia walipopitia hapo.

122 Naye mwangalizi huyo angesimama pale. Hapo . . . Vema, zetu zilikuwa ni Turkey Track, na ya jirani ilikuwa Tripod, Diamond Bar, na Grimes walitufuata; na wote juu chini kule, aina zote mbalimbali za chapa zilipitia pale. Lakini mnajua nini? Mwangalizi huyo kamwe hakuvutiwa na hiyo chapa. Labda angeitupia jicho na kuangalia kando kando, bali hiyo haikuwa ndiyo. Kamwe hakuiangalia hiyo chapa, bali bila shaka alichunguza kibandiko cha damu. Hapakuwapo na ng'ombe

angaliweza kuingia kwenye malisho hayo isipokuwa alikuwa ni Herefodi aliyesajiliwa.

123 Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye Kizimba cha Hukumu. Yeye hatakuuliza kama wewe ni mfuasi wa Church of God, Assemblies of God, ama Pentecostal Holiness, ama kama wewe ni wa Umoja, Uwili, Utatu, Unne, Utano, au chochote ulicho. Yeye ataangalia kile kibandiko cha Damu. Na hicho ndicho kitakachokuingiza ndani, itakuwa ni ile Damu. "Nitakapoiona hiyo Damu, nitapita juu yako." Hiyo ni kweli kabisa, ndugu, mnaona. Hiyo ni kweli.

124 Kwa hiyo tukirudi nyuma, sasa, tunaona ya kwamba kulikuwako na kongamano. Walikuwa wamesahau yote kuhusu. . .Walipata. . .Musa aliingia kwenye kanuni zake za imani huko nje na kuusahau ule mzigo. Lakini Mungu alichagua mahali Naye akafanya kongamano. Naye akamwita Musa. "Vua viatu vyako Musa, uko kwenye mahali patakatifu. Nimesikia vilio vya watu Wangu. Nimekumbuka ahadi Zangu nilizofanya na Ibrahimu, nami nitakutuma huko ukawakomboe."

125 Sasa, Musa alijua Sauti hiyo ilikuwa ni Mungu, kwa sababu ilikuwa ni ya Kimaandiko. Sasa, mtu yeyote ambaye—ambaye anapita na kuiona sauti, na kama ni ya. . .wao. . . si sauti ya Kimaandiko, achana nayo; kama Biblia ikisema hivyo, basi iamini, kwa sababu ni Sauti ya Kimaandiko. Watu wakisema "malaika" na kadhalika, Joseph Smith aliona mmoja. Ninatofautiana na Joseph Smith, kwa sababu haikuwa ni ya Kimaandiko, bali sisemi mtu huyo kamwe hakumwona malaika. Sipaswi kulipinga neno la huyo mtu. Kumekuwako na malaika wengi, na kadhalika, walioonekana. Bali kama malaika yeyote. . .Paulo alisema, katika Wagalatia 1:8, "Kama malaika kutoka Mbinguni akija, akahubiri injili nyingine yoyote isipokuwa ile nimewahubiri tayari, na alaaniwe." Hiyo ni kweli. Dumu na hilo Neno; moja kwa moja na hilo Neno; na yale Neno lisemayo, dumu moja kwa moja nayo. Usiondoke hapo.

126 Naye Musa akaona kwamba kongamano ambalo alikuwa akifanya na Mungu, ama Mungu alikuwa akifanya naye, lilikuwa ni la Kimaandiko kabisa, kwa sababu Mungu alifanya ahadi Naye akasema angewakomboa. Na Mungu akasema, "Nilikuchagua, Musa, nawe utashuka uende ukafanye hivyo." Musa anashuka moja kwa moja na kuingia Misri na kufanya miujiza ambayo Mungu alimwambia. Hatuna wakati wa kuingilia hilo kama vile ningetaka kufanya, lakini mnaelewa.

127 Wakati aliporudi, akiwatoa wana wa Israeli akiwapeleka kwenye nchi ya ahadi, moja kwa moja kwenye mapito ya wajibu kulikuwako na Bahari ya Shamu. Ni ajabu vile Mungu atakavyowaongoza watoto Wake moja kwa moja kwenye mitego; wakati mwingine viti vya magurudumu, wakati mwingine na mishtuko ya moyo, wakati mwingine Yeye huwaongoza

watoto Wake. . .Kwa nini? Kuona vile watakavyotenda, kuona vile. . .aone watakuwa na tendo gani kwenye tendo, aone kile watakachofanya.

128 Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa, kupimwa. Katika Agano la kale mwana alizaliwa katika familia, lakini i—ilibidi afunzwe na kulelewa na kujaribiwa. Ndipo aliwekwa kama mwana, ama kufanywa mwana mwenye mamlaka, akawekwa kwenye mwili, ama katika. . .Basi wakati alipowekwa, mara alipowekwa, basi jina lake lilikuwa zuri tu kwenye hundi kama la baba yake lilivyokuwa. Yeye alikuwa mrithi wa vitu vyote. Hapo ndipo Mungu anapolileta kanisa Lake, akiwapa majaribu.

129 Hiyo hapo Bahari ya Shamu moja kwa moja kwenye mapito ya wajibu wao. Wangefanya nini? Sasa, ilionekana kana kwamba maumbile yote yalikuwa yakiwalilia. Hapo lilikuwapo jeshi la Farao likija, yale magari. Hapa ilikuwapo milima pande zote mbili. Bahari ya Shamu ilikuwa imewanasa. Ilionekana kana kwamba ilikuwa ni. . .ilionekana kana kwamba maumbile yangepiga mayowe, pamoja na jeshi hilo kuu la watu milioni mbili na nusu huko chini bondeni, hawajiwezi, hawana panga, hakuna kitu cha kupigana nacho. Kwa hivyo nini kilitendeka? Kulikuwako na hali ya dharura, ndipo Musa akachagua mwamba fulani akaenda nyuma yake na kuitisha kongamano. Ninapenda hilo. "Nifanye nini, Bwana?"

130 Si lingekuwa ni jambo zuri kama makanisa yote yangeitisha kongamano sasa hivi? Tunapoona jinsi mambo yanavyoendelea, kama tusingaliitisha kongamano, na kutambua na kurudi nyuma na kutaka kujua ni kanisa la namna gani Mungu alilokuwa nalo hapo mwanzo? Tuitishe kongamano na kusemezana pamoja mmoja na mwenzake? Tuone yale kanisa la kwanza liliyofanya, ni Roho wa namna gani aliyekuwa ndani yao, na ni ishara za namna gani zilizowafuata, ni huduma ya aina gani waliyokuwa nayo, walikuwa watu wa aina gani? Si lingekuwa ni jambo zuri sana kama tungefanya hivyo? Lingekuwa ni jambo zuri sana!

131 Musa alifanya hivyo. Alitambaa nyuma ya mwamba mahali fulani, na kusema, "Bwana, nifanye nini? Hawa hapa watu hawa. Mimi niko moja kwa moja kwenye wajibu. Nilifanya yale hasa uliyoniambia nifanye. Nami huyu hapa nimekabiliwa na hili moja kwa moja."

132 Labda umeketi hapa usiku wa leo, maskini mama mzee, ambaye amelea kundi la watoto. Ukawalea kadiri alivyofanya Susanna Wesley. Yeye alikuwa na watoto kumi na saba, hata hivyo angeweza kupata saa tatu kwa siku kuomba na kuwaelekeza kwa Mungu. Hiyo ndiyo sababu alikuwa na Charles na John. Siku hizi tunabonyeza kitufe, tunaosha vyombo; tunabonyeza kitufe, tunafua nguo; wala hatuna wakati kwa ajili

ya chochote. Mnaona, kuna kasoro mahali fulani; sasa, loo jinsi ibilisi anavyoweza kuwafanya watu.

133 Angalia, lakini sasa walikuwa na kongamano hili, naye Musa akamtaka Mungu shauri. Alingojea pale mpaka akapata maagizo, kama vile Adamu alivyofanya. Alingoja mpaka kukatolewa maagizo ya jambo la kufanya. Musa alingojea mpaka akapata maagizo kama alivyofanya huko juu. "Ati nini . . .? Nitawakomboaje? Nifanye nini?"

"Shuka uende ukawaambie, MIMI NIKO amekutuma." Hilo lilitosha.

134 Sasa, hapa yeye yuko tu moja kwa moja kwenye wajibu wa agizo tena, moja kwa moja kwenye wajibu, ndipo adui anatokea. Labda amekuja kwako, labda juu yako, labda juu yako wewe, wewe, wewe, kila mahali hapa. Ugonjwa wa moyo; maradhi; mateso mwilini mwako; unaweza kufanya nini? Umeomba vya kutosha? Kila kitu ni sawa? Basi hebu tufanye kongamano. Amina! Hebu tutafute kujua la kufanya.

135 Unasema, "Ndugu Branham, nimejaribu kumpata Roho Mtakatifu. Nimemtafuta Mungu, nimemtafuta Mungu, wala siwezi kumpata Roho Mtakatifu."

136 Hebu tufanye kongamano basi tuone kuna shida gani. Roho Mtakatifu ndiye Mfunuzi wa siri za moyo. Biblia ilisema hivyo. Hebu tuone kuna shida gani. Hebu tuone ni kwa sababu gani wewe humpati Roho Mtakatifu. Tuone shida ni nini. Hebu tufanye kongamano.

Musa alikuwa na kongamano, naye alingojea mpaka akapata maagizo.

137 Ninapinga mengi ya huu hapa uponyaji wa Kiungu wa ajabuajabu walio nao nchini siku hizi. Huenda msinipende baada ya tamshi hili, lakini, nitalisema hata hivyo. Wana upuuzi mwingi sana wa ajabuajabu. "Loo, uponyaji wa Kiungu, kila mtu, jambo pekee likupasalo kufanya ni (Haleluya!), ni kwamba waweke mikono yao juu yako, utukufu kwa Mungu!" Hivyo sivyo. Tubu, na ukajiweke sawa na Mungu! Hilo ndilo tunalohitaji: toba zaidi.

138 Nilisoma barua kutoka kwa kanisa la Kilutheri sio muda mrefu uliopita. Sisemi hili kwa kujisifia, Mungu anajua hilo moyoni mwangu, juu ya Biblia hii. Alikuwa kweli akimrarua vipande-vipande mmoja wa hao wainjilisti kuhusu baadhi ya mawazo yao ya ajabuajabu ya uponyaji. Kasema, "Vipi kuhusu maskini Deborah Stadsklev, wakati mama huyo alipoendesha gari hapa na alikuwa amesimama pale wakati . . . "

139 Maskini mtoto huyo mchanga alikuwa . . . alikufa usiku huo, na hii ilikuwa kesho yake alasiri. Amekufa, daktari alitangaza amekufa na kila kitu; baridi na amekauka. Akawekwa mikononi mwangu nami nikamwombea. Huyo mtoto akapata, analia;

nikamrudisha mikononi mwa mama yake. Mama huyu alikuwa amesimama pale kuona hilo. Yeye aliandika wakati mtoto wake mchanga aliposhikwa na ugonjwa huko Ujerumani, Bibi Stadsklev, Kapteni Julius Stadsklev, yeye ni rafiki wa Billy Graham, mmoja wa washirika wangu mkutanoni, aliandika kitabu hicho mnachokipata hapa sasa, *Nabii Azuru Afrika*. Na sasa . . . naye alikuwako kule wakati Malaika wa Bwana alipokuja nao wakampiga Yeye picha, Nguzo hiyo ya Moto iliyoshuka, huja mikutanoni. Yeye alipiga picha ya huyo: akayaona yote.

140 Na kwa hiyo yeye . . . wakati mtoto wake mchanga alipokufa, maskini mama huyo asingepata amani yoyote. Akapiga simu kutoka Ujerumani, na shirika la ndege la Jeshi la Anga la Marekani lilikuwa linisafirishe kwa ndege hadi Ujerumani. Kasema, "Mtoto huyu mchanga anaweza kufufuliwa tena."

141 Nikasema, "Hebu nione yale Bwana asemayo." Nami nikangojea, na kungojea. Siku mbili zikapita. Huyo daktari alikuwa ni mzuri sana. Hata hawakuninii . . . walikuwa nao huko wakipiga makelele juu ya huyo mtoto, na kupiga mayowe na kufanya makelele namna hiyo, na kila kitu, bali hakuna uhai. Nikaendelea kungoja.

142 Asubuhi moja Roho Mtakatifu akaniamsha na kusema, "Kamwe usiliguse hilo, usilikemee. Huo ni mkono wa Bwana." Nami nikawatumia ujumbe.

143 Huyo mhudumu Mlutheri akasema, "Kwa nini hukungoja namna *hiyo* mpaka upate uamuzi dhahiri kutoka kwa Mungu?" Ndipo unajua mahali unaposimama. Ngoja mpaka utakapokuwa na BWANA ASEMA HIVI, ndipo ujue mahali ulipo.

144 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . nywele . . . Kitu fulani kilienda kombo mahali fulani. Kitu fulani kilienda . . . Hakika wanafanya hivyo sasa. Wanasema ni kuumwa na kichwa. Vema, ndugu, hakupaswi kuweko na kuumwa na kichwa nchini basi. Naam, ndiyo, bwana. Kuna kasoro mahali fulani.

145 Pia ilikuwa ni kosa kwa wanawake Wapentekoste . . . Sijawa kwenye huduma ya Kipentekoste ila kwa muda mfupi tu, lakini ninaliona tu likikua polepole, likipanuka, likifanyika . . . Mmeangalia televisheni nyingi kupita kiasi, upuuzi mwingi mno ambao hampaswi kuangalia; badala ya kufanya mikutano ya maombi na kulirudia kanisa la Mungu, siku hizo za maombi ya usiku kama walizokuwa nazo. Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho.

146 Mungu angeweza kumtuma Oral Roberts fulani, Tommy Hicks fulani, na *nanii*, kote nchini, na bado hatuna kitu cha kujengea juu yake, mpaka tutakaporejea kwenye ule uamsho wa kale wa Mtakatifu Paulo na kumwamsha Roho Mtakatifu kurudi kanisani tena. Mashemasi kanisani waliooa mara nne ama tano na kila namna ya upuuzi, wakati mkijua hiyo si Biblia. Amina.

147 Nilimwambia mama mmoja hivi majuzi. . . Yeye alisema, “Nakwambia, mimi sivai maskini kaptura hizo.” Kasema, “Mimi huvaa suruali ndefu.”

148 Nikasema, “Hizo ni mbaya zaidi.” Kweli. Naam, yeye ni. . . Ni mbaya! Biblia ilisema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume. Huo ni uchafu. Naam. Mwanamke fulani alisema hawatengenezi nguo zingine tena. Wangali wanatengeneza cherahani nawe unaweza kununua kitambaa. Hakuna udhuru. Unachohitaji ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mtindo wanaoanzisha ni dhihaka. Amina. M—mnafikiri nimerukwa akili, bali sivyo. Ninajua mahali nilipo hasa. Um-hum. Hiyo ni kweli. Naam.

149 Wanavaa jinsi hiyo na kuingia mtaani. Huenda ukawa mwadilifu kwa mumeo uwezavyo kuwa, huenda ukawa binti mwadilifu sana kwa mpenzi wako uwezavyo kuwa, bali kwenye Siku ya Hukumu utawajibika kwa ajili ya uzinzi. Utakuwa na hatia ya kufanya uzinzi. Yesu alisema, “Yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Ulijianika hivyo naye mwenye dhambi akakuangalia. Wakati akiwajibika kwa ajili ya uzinzi, ni nani mwenye hatia? Wewe, kwa kujianika namna hiyo. Amina.

150 Sasa, hiyo ni kweli. Msinikasirikie sana. Hilo ni Neno la Bwana. Loo, tunachohitaji ni kongamano katika Pentekoste. Naam, bwana. Kweli kabisa, turudi kwenye kongamano la Kipentekoste.

151 Tunaona Musa alisimama pale hata Mungu akampa maagizo. Ndipo alipotoka nyuma ya mwamba huo, ningemwazia akisema, “Haya tusonge mbele.”

Baadhi yao wakasema, “Twende mbele wapi?”

152 “Endeleeni tu kusonga mbele, hivyo tu.” Wakati mguu wake ulipoyagusa maji, Bahari ya Shamu ilirudi nyuma nayo nchi kavu ikatokea. Naye akatembea kupitia nchi kavu, maana alifanya kongamano na Mungu.

153 Loo, kunayo makongamano mengi tunayoweza kunena habari zake. Kulikuwako na kongamano la—la tanuru iliyowaka moto, kulikuwako na kongamano katika tundu la simba. Tumekuwa na makongamano mengi.

154 Hebu tuliendee lingine. Linaitwa “Kongamano la Gethsemane.” Hilo hapo lilikuwa ni kongamano la kutisha mno. Haikumbidi kufa kijana Mwanamume. Haikumbidi kufanya hivyo. Lakini alipowaona binadamu waliopotea katika hali yao, kasema, “Si mapenzi Yangu bali Yako yatendeke.” Malaika walikuja wakamhudumia. Hiyo ndiyo. . .

155 Ndipo baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, ilibidi kuwe na kongamano lingine: jinsi ambavyo kanisa la Kikristo linapaswa kuendeshwa. Um-hum. Kama linapaswa

kuongozwa na maaskofu, ama kama linapaswa kuongozwa na mapapa, ama jinsi linavyopaswa kuongozwa. Kwa hiyo Yesu akawaambia katika Luka 24:49, "Ngojeni tu huko juu katika mji wa Yerusalemu. Ninapaa juu kufanya kongamano na Baba. Nitawatumia Neno baada ya kitambo kidogo, bali ninyi ngojeni huko mpaka nyinyi . . . Nitawaambia jinsi linavyopaswa kuendeshwa." Kama Petro atakuwa ndiye papa wa kwanza au la, um-hum, um-hum, kama tutakuwa na maaskofu na maaskofu wakuu na wazee wa jimbo na kila kitu kingine.

"Tutafanyaje jambo hilo? Tutangojea tuone."

156 Ndipo wakawa na kile wanachokiita "Kongamano la Kipentekoste." Wakapanda maskini hivyo vipandio vidogo vya nje vya kwenda juu, wakaingia kwenye chumba cha juu ambamo watu mia moja ishirini walikusanyika; maskini taa ndogo ya grisi ikiwaka. Hawakula wala kunywa kwa muda wa siku kumi, wakingoja. Matokeo ya hilo kongamano yalikuwa nini? Lilikuwa ni refu sana. Nao walikuwa na siku kumi za kungojea, ndipo baada ya kitambo kidogo matokeo yakaja. A-ha, a-ha. Loo, naam.

157 Hapakuwapo na kasisi aliyepanda barabarani huku ukosi wake umepinduliwa na kusema, "Sasa, tutakula komunio ya kwanza. Wewe toa ulimi wako nikupe mkate mwembamba, nami nitakunywa divai." Hiyo si ingekuwa . . . ?

158 Wala hapakuwapo na mhubiri aliyepanda kuja barabarani na kusema, "Tupe mkono wa kulia wa ushirika. Tutaandika jina lako kwenye kitabu na kukujaribu kwa muda wa miezi sita ya majaribio." La. Hayo ni makongamano ya binadamu. Hivyo ndivyo wanavyofanya kwenye mabaraza na makongamano.

159 Ni jambo gani lililotukia? Wakati matokeo ya hilo kongamano yalipokuja, wote walikuwa mahali pamoja na moyo mmoja, ndipo mara ukaja uvumi kutoka Mbinguni kama upepo wenye nguvu ukienda kasi, na ukakijaza chumba chote walimokuwa wameketi. Ndimi zilizogawanyika zikawakalia kama moto, nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha zingine kama Roho alivyowajalia kutamka. Hayo yalikuwa ndiyo matokeo kutoka kwenye makao makuu. Roho Mtakatifu alikuwa aliongoze kanisa, sio mafundisho ya sharti ya kujibunia, bali Roho Mtakatifu. Hilo lilikuwa ndilo Kongamano la Kipentekoste.

160 Nami nafikiri kote kote kutoka Martin Luther mpaka Pentekoste wanapaswa kurudi wafanye kongamano tena, wapate kujua, ni Roho Mtakatifu ndiye anayepaswa kuliongoza kanisa, si mafundisho ya sharti, na kanuni za imani, na *Salamu Maria* na Kanuni ya Imani ya Mitume. Ninawatakeni mnitafutie Kanuni ya Imani ya Mitume katika Biblia. A-ha. Hakuna kitu kama hicho; bali hata hivyo tunaiinamia, na kuikariri, na kama tu . . . Hao ni wajiungao na chama; hao si Wakristo.

161 Wakristo wanazaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Roho Mtakatifu anaingia ndani yao, nao wanajazwa na Roho. Uzima wa Kristo unaishi kupitia kwao. "Wanaenda ulimwenguni kote na kuihubiri injili." Umbali gani? Ulimwenguni kote. Kwa ajili ya kizazi hiki tu? Ulimwenguni kote. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Umbali gani? "Ulimwenguni kote, kila kiumbe kinachoamini." "Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, wakishika nyoka, ama wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

162 Hivyo ndivyo maagizo yalivyokuwa. Hayo yalikuwa ndiyo maagizo kutoka kwenye hilo kongamano, kutoka kwa Mungu Mbinguni, akashusha chini matokeo, upepo wenye nguvu ukienda kasi. Loo, umbali gani...? Tunahitaji kongamano lingine, ndugu.

163 Kulifanyika nini wakati lile kongamano? Hawakutembea huko na kusema, "Sasa nauchukua mkono wako. Nitakuwa mfuasi wa kanisa hili."

164 Achukue kitikisa chumvi na kurusha minyunyizo mitatu au minne ya ma-...chafu, ama maji, chochote unachotaka kuyaita, juu yao na kutoka nje na kusema, "Sasa wewe ni mfuasi." Hilo si sawa. La bwana.

165 Hata si kwa ubatizo wa maji, ambao ni muhimu sana: ungali ulikuwa sio kitu hicho.

166 Lakini ulikuja uvumi, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ulikuja kutoka Mbinguni. Ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Hayo yalikuwa ndiyo matokeo ya kongamano hilo, jinsi ambavyo Mungu aliamua kuliendesha Kanisa Lake. Tunathubutuje kujaribu kuondoa nukta moja kutoka kwa hiyo! Tunathubutuje, kama wanadamu, kuongeza jambo moja ama kuondoa jambo moja kutoka kwake? Tunawezaje kufanya hivyo? Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuendeshwa: kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

167 Kulikuwako na kongamano lingine lililofanywa mara moja. Hao watu walienda, wakahubiri Injili, wakawaponya wagonjwa. Petro na Yakobo walipitia kwenye lango liitwalo Zuri, na hapo alikaa kiwete toka tumboni mwa mamaye. Kasema, "Fedha na dhahabu sina, ila nilicho nacho, nitakupa: Katika Jina la Yesu Kristo simama uende." Naye huyo akaenda.

168 Basi nini kilichotukia? Walitaka kuwaweka gerezani. Makala ya habari yalikuwa na ukosoaji wa kila namna ndani yake. Nao waliwakosoa tu na kuwapokonya mbele ya lile baraza, baraza kuu la kanisa. Wakati walipofanya hivyo kwenye baraza la Wazee, waliwakataza kuhubiri Injili ya aina hiyo tena. Kwa hiyo iliwabidi kufanya nini? Walikatazwa kulihubiri Jina la Yesu Kristo. Kwa hiyo wangefanya nini? Wakafanya kongamano

lingine: "Kongamano la Matendo 4" tutaliita hivyo, Matendo 4. Wakakusanyika pamoja na kundi lao wenyewe.

169 Hilo si lingekuwa ni zuri endapo Wakristo wote wangekusanyika na makundi yao wenyewe, na makundi yote yangekusanyika pamoja na kufanya kongamano, "Tufanye nini?" Ukomunisti unalipenya taifa letu, taifa letu limeanza kupenyezwa na ukomunisti; nalo kanisa linakuwa baridi na la kidesturi za dini. Makanisa yanapigana yenyewe kwa yenyewe, yakilipuana, nao washirika wana . . .

170 Ungeweza kuwauliza ikiwa wao ni Wakristo. Waseme, "Mimi ni mfuasi wa *Hiki-na-hiki*." Hilo halina uhusiano wowote nalo. Mungu hajali *hilo* kuhusu dhehebu lako. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.] Yeye anataka kujua kama umezaliwa mara ya pili. Endapo hujazaliwa mara ya pili, basi wewe si Mkristo. Unaweza tu kuwa Mkristo wakati unapouchukua Uzima wa Kristo ndani yako. Kama Uzima wa Kristo uko ndani yako, utazaa Uzima wa Kristo. Unaweza kukusanya mapichi kutoka kwenye mmea wa tikitimaji? Bila shaka huwezi.

171 Kwa hiyo angalieni lililotukia. Walikusanyika, wakakutana pamoja, nao wakanukuu Maandiko, wakayarudia Maandiko kwa Mungu. Kasema, "Mbona makafiri wamefanya ghasia na makabila wametafakari ubatili?" Telepathia, kupiga ramli, kusoma mawazo, ubatili huu wote, kasema, "Kwa nini wanatafakari ubatili? Kweli, unyoshe mkono Wako, wa Mtoto Wako mtakatifu Yesu, kuponya."

172 Basi wakati walipofanya kongamano hilo, na kulikuwako na yapata . . . nadhani kulikuwako na elfu tatu walioongoka kwenye siku ya Pentekoste, na—na mamia na mamia mengi baada ya hapo. Labda walifikia, katika watu elfu nane ama elfu kumi, wamekusanyika chumbani kuomba. Ndipo walipofanya hivyo, na kuomba wote kwa moyo mmoja, wote wakati uo huo, Biblia ilisema ya kwamba jengo lilitikisika ambamo walikusanyika pamoja. Jibu likaja, nayo Biblia ilisema walihubiri Neno la Mungu kwa ujasiri.

173 Watu wengine wanaogopa kulihubiri Neno. Wangefukuzwa kanisani mwao, dhehebu lao. Wanaogopa hilo. Basi tunahitaji kongamano lingine, Kongamano la Matendo 4. Unahofia yale mtu mwingine atakayosema? Maadamu Mungu alilisema, dumu pamoja nalo; ishi nalo, kufa nalo. Kweli. Nawe utafufuka nalo, jambo pekee utakalofanya, njia pekee unayoweza kufufuka.

174 Kongamano, tunachohitaji ni kongamano. "Njoni, tusemezane," asema Mungu. "Kama kanisa Langu la kwanza . . ." Lingesema, Mungu angekuja chumbani usiku wa leo na kusema, "Kama nililichagua Kanisa Langu la kwanza nao walikuwa na baraka za Pentekoste juu yao, na yale waliyofanya, walitoka wakaenda na kuonyesha ishara za kule kufufuka; hebu tuje tukasemezane ni kwa nini hatuna

hayo usiku wa leo katika makundi yetu ya Kipentekoste, katika makundi yetu ya Methodisti, katika makundi yetu ya Baptisti, katika makundi yetu ya Presbiteri. Kuna shida gani? Kuna kasoro fulani. Kwa hiyo hebu tuje, tukasemezane."

175 Tungewezaje kusemezana? pamoja na—pamoja na Wamethodisti? pamoja na Wabaptisti? pamoja na Presbiteri? La, bwana. Tunaweza tu kusemezana kwa Neno la Mungu. Nalo kanisa la kwanza lilijazwa kwa Roho Mtakatifu, likatoka likaenda katika ishara kuu na maajabu. Maisha ya Yesu Kristo yalijionyesha Yenyewe katika maisha ya kila mmoja wa watu hao. Hebu tuje . . . mbona . . .

176 "Haya tusemezane," asema Bwana. "Haya tuje, na kusemezana. Ingawa dhambi zako, kutokuamini kwako, ni kwekundu sana, nitakufanya kweupe kama theluji. Zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu. Nitawapa uamsho. Nitairudisha miaka yote iliyoliwa na madumadu, iliyoliwa na nzige. Yaliyosazwa na Lutheri, yameliwa na Methodisti. Yaliyosazwa na Methodisti, yameliwa na Baptisti. Yaliyosazwa na Baptisti, yameliwa na Pentekoste. Lakini nitarudisha," asema Bwana. Hmm. "Nitaninii . . . "

177 Ni hakikisho la kurudishwa, hilo ni jambo moja. Mungu aliliahidi katika Yoeli 2. "Haya njoni, tusemezane." Yale mmoja aliyokula na kusaza, huyo mwingine aliyachukua kote kote, mpaka ikawa ni kisiki. Pentekoste, kanisa halisi la Kipentekoste, watu halisi wa Kipentekoste, ujuzi halisi wa Kipentekoste umeanza . . . ni jambo la kihistoria.

178 Sasa, ningewezaje kusimama na kuwafundisha thiolojia? Ingefaa nini mimi kuwaambia ya kwamba Mungu wakati mmoja aliwaponya wagonjwa, na—na kuwafanya viwete kutembea na vipofu kuona; na kuimwaga Roho Yake, nao walikuwa na utambuzi wa roho, na wakafanya mambo haya yote; na ishara ya Masihi, ufufuo, iliwafuata kupitia wakati wa kanisa; kisha niwaambie siku hizo zimepita? Mungu wa historia anafaa nini, kama Yeye si Mungu yeye yule leo?

179 Ingefaa nini kuwapa ndege wako wa kurumbizi vitamini kukuza manyoya mazuri na mifupa ya bawa yenye nguvu, kisha umweke kwenye kizimba? Shule ya thiolojia inafaa nini, kama huwezi kumwacha mtu huyo ajue ya kwamba Mungu angali Mungu? Kama Yeye ni kitu tu cha kihistoria, Yeye ni wa siku zilizopita.

180 Lakini Yeye hajafa; Yu hai milele. Yupo hapa sasa. Yeye ni Kristo. Bila shaka.

181 Tunapaswa kukusanyika na kusemezana. Lilikuwa ni kanisa la aina gani hapo mwanzo? Hiyo ndiyo aina ya kanisa . . . Mungu hana kikomo na hawezi kubadili nia Yake. Mungu anapofanya uamuzi, Yeye hana budi kuudumisha. Uamuzi Wake wa kwanza wa kanisa halisi la Kikristo ulitokea kwa tukio la Kipentekoste.

Sasa, hilo halikuwa ni dhehebu la Kipentekoste; hilo lilikuwa ni tukio la Kipentekoste, linaloweza kuja kwa Mmethodisti, Mbaptisti, Mkatoliki, Mpresbiteri, ama yeyote atakaye. Hilo ni tukio linalokuja.

182 Upendo, upendo wa Mungu. Upendo ndio kitu chenye nguvu kuliko vyote kilichoko ulimwenguni. Hushinda chochote, ni upendo. Kwa huu utashinda, kwa upendo wa Kiungu, kupendana, kuipenda huduma ya Mungu, kumpenda Kristo, kuwapenda wanadamu wanaoteseka. Hivyo ndivyo unavyoshinda.

183 Naam, walikuwa na kongamano, nao wakapata maagizo, kisha wakaondoka, nao wakamhubiri Mungu wa. . .Neno la Mungu kwa ujasiri.

184 Sasa, nitazungumza juu ya kongamano moja zaidi kwa muda kidogo tu. Huenda ulikosa Kongamano la Geneva. Huenda hata hukusikia matokeo kwenye redio. Huenda ulilikosa lile la Gethsemane, ambalo ulilikosa. Huenda ulilikosa la Bahari ya Shamu. Ulilikosa. Huenda uliyakosa makongamano haya yote, bali hili hapa moja ambalo utasimama, hilo ni kongamano kwenye Hukumu. Nyote mtakuwa kule. Kila mmoja wetu atasimama kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo kutoa hesabu ya yale tumefanya na Kristo pamoja na Neno Lake.

185 Kutakuwako na kongamano, nawe utakuwa pale. Sijali unayofanya na maisha yako. Ungeweza kujinyonga, uwe na hatia sana hata mwili wako uchomwe moto na kupelekwa huko baharini na kupuliziwa kwenye pepo nne. Utakuwa pale kwa vyovyote vile, kwa kuwa kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri. Huenda kumekuwa na kongamano kubwa mno, na mengi ya hayo ambayo ungeyakosa; bali kuna moja utakalohudhuria.

186 Nami nitakwambia, kila unapoona nywele zenye mvi inamaanisha ya kwamba unaenda. Kila unaposikia king'ora, wewe ni. . .ni kongamano utakalokabiliana nalo. Mauti yanakukabili uso kwa uso. Kijana ama mzee, hata uwe nani, uko njiani mwako. Kila wakati unapopitia makaburini, inanena ya kwamba unakuja kwenye kongamano hilo. Kila wakati unaposikia mahubiri yakihubiriwa, wimbo ukiimbwa, inamaanisha unakuja kwenye kongamano hilo, nawe utakuwa kule. Nawe utawajibika kwa yale umefanya na Neno la Mungu, pia na Mwana wa Mungu, vile vile na Roho Mtakatifu ambaye Yeye alikutumia. Utawajibika. Utakuwa kwenye kongamano hilo.

187 Kwa hiyo kama mpo hapa usiku wa leo, enyi marafiki, na hamjawahi kuwa na kongamano hilo pamoja na Mungu. . . Dhambi za watu wengine huwatangulia, zimeungamwa; za wengine huwafuata. Kama zako, kutokuamini kwako, hakujaungamwa bado, mbona usiwazie hilo wakati tukiomba, tunapoviinamisha vichwa vyetu?

188 Katika uchaji na kicho cha muda huu ningeuliza swali la kicho ambalo itawabidi watu wote kujibu. Iweni waaminifu, na hebu huu uwe ni wakati wa kujichunguza moyoni mwako. Utafanya nini baada ya kongamano *hili*?

189 Hili ni kongamano usiku wa leo, ambapo tumekusanyika hapa kwenye ukumbi huu wa michezo ya viungo kuzungumzia Neno la Mungu katika kumbi na kadhalika kama tu walivyofanya katika siku za mwanzoni. Neno lile lile la Mungu limehubiriwa. Itakubidi kuwajibika kwake siku moja.

190 Kunao wale hapo. . .hapa usiku wa leo, ama ni wangapi? (Ninajua kunalo kundi) ambalo lingeniambia jambo hili: "Ndugu Branham, sijawahi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu. Sijawahi kumpokea Roho Mtakatifu wa Mungu. Nami najua kama nikisimama kwenye lile—lile kongamano, nikiisha kuambiwa dhahiri sana na Maandiko, nikashuhudiwa na Roho Mtakatifu, itanibidi kutoa hesabu ya maisha yangu kwenye siku ile. Nitamwinulia Mungu mkono wangu na kumwomba anirehemu, nami ninataka kongamano sasa hivi pamoja na Mungu. Ningetaka kulizungumzia pamoja Naye sasa hivi."

191 Sasa, huku kila kichwa kimeinamishwa (Walaaniwe watakaoyainua macho yao.), ungeweza kuinua mkono wako na kusema, "Niombee, Ndugu Branham. Bado sijampokea Roho Mtakatifu"? Mungu akubariki. Mtu mwingine? Hakika ungekuwa mwaminifu kwenye wakati kama huu; kwenda kwenye kongamano. Mungu akubariki, mama, Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki wewe *hapa*.

192 Unaelekea kwenye kongamano. Pia kumbuka, haidhuru umekuwa mwema jinsi gani kanisani, hilo hali-. . .hilo halifanyi jambo lolote. Mafarisayo katika siku za Yesu waliishi maisha matakatifu zaidi kuliko yeyote wetu hapa Marekani anavyoishi; bali walihesabiwa kuwa waovu, kwa sababu walikuwa ni wenye dhambi, wasioamini katika Kristo na Neno Lake. Nami nimewaambia dhahiri lile kongamano, wakati Mungu alipotaka kuamua alitaka kanisa la aina gani, lilikuwa ni kanisa lililojazwa na Roho kutoka Pentekoste. Endapo hujakutana na kongamano hilo bado, waweza kuinua mkono wako na kusema, "Ndugu Branham, niombee"? Mungu akubariki wewe, wewe, wewe.

193 Katika roshani mkono wangu wa kushoto, kunaye yeyote huko juu ungeinua mkono wako kwa utulivu? Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mtu akiomba, tafadhalini. Roshani upande wa kushoto, roshani upande wa nyuma, roshani upande wa kulia; sasa kumbukeni, siwezi kuwafanya mfanye hili, ninaweza tu kunena Neno, ni juu yenu kuamua. Ila kumbukeni, ujumbe uu huu utawahukumu. Uko kwenye kanda ya sumaku Mbinguni, nayo itachezwa tena kwenye Siku ya Hukumu.

194 Endapo hujampokea Roho Mtakatifu wa Mungu bado, kamwe hujawa na kongamano hilo na kukutana kama walivyofanya kwenye kongamano la Kipentekoste, hujawahi kumpokea bado, inua tu mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Mtu fulani ambaye hajainua mkono wao kwa Mungu, inua mkono wako.

195 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unaiona hii mikono ya hawa watu. Kulikuwako na wengine ambao waliinua mikono yao nao walitaka kukumbukwa kwa maombi, ujasiri tosha. Jinsi wanavyopaswa kuwa wenye shukrani. Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Wazia juu ya wale tunaowajua wanaoketi papa hapa ambao hawakuinua mikono yao. Sasa, Wewe ni Mtambuzi wa moyo. Wale ambao ulinena nao wala hawakuinua mikono yao, itakuwaje kwa hao watu kwenye hiyo Siku ya Hukumu hapo kongamano la mwisho litakapofanywa? Ndipo itaamuliwa ni nani ambaye alipokea, na ni nani hakupokea, ambao majina yao yalikuwa kwenye kile Kitabu. Wewe ulisema, "Wale walio kwenye mkono Wangu wa kushoto, nitasema, 'Ondokeni mkaingie katika moto wa milele ambao ulitengenezewa ibilisi na malaika zake.'"

196 Nasi tunajua ya kwamba wakati umekaribia. Tunaona ulimwengu katika hali ya kutikisika, kutetemeka; tukijua ya kwamba atomi hivi karibuni zitakuwa zikiungua, mbingu zitawaka moto, kama vile mtume Petro alivyosema, nao utateketea kwa moto mkali. Atomi za duniani zitashika moto hivi karibuni. Kutakuwako na kubadilishana, wala hapatakuwapo hata na mavumbi ya watu yatakayosalia.

197 Halafu nini, Bwana? Labda miaka mia tano kutoka sasa jiwe la kale la kaburini, lililopuliziwa huko ng'ambo katika pepo zivumazo, jua kali sana, linalowaka, wakati likiwa karibu na jua kwa ajili ya kutakaswa kabla ya ule Utawala wa Miaka Elfu, labda jina la baadhi ya watu hapa litakuwa limeandikwa kwenye hilo. Nafsi zao zinazozurura zitakuwa wapi? Jalia wasiuangalie ulimwengu huu mamboleo sasa, bali jalia waangalie aliko Kristo, wausikilize ujumbe na Mjumbe anayenena moyoni mwao. Wabariki wale walioinua mikono yao, Baba, jalia wampokee Roho Mtakatifu, naomba, katika Jina la Kristo.

198 Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kwa muda kidogo tu, hivi kweli ulimaanisha hilo? Waweza kuja hapa madhabahuni? Simama kutoka kitini mwako sasa, wewe uliyeinua mkono wako.

199 Na nyinyi ambao hamkuinua mikono yenu: kama mmekuwa kwenye mikutano ya usoni, ambayo mtaiona hapa, pia, mumwone Yeye kwa maombi akiyafungua macho ya watu walio vipofu, mumwone Yeye akiwaponya hao walio viwete na wamepindapinda, mumwone Yeye akishuka chini na

kuyatambua mawazo yenyewe ya moyo wa watu, kama tu Yeye alivyosema . . .

200 Sasa, huyo ni Roho Wake ambaye anazungumza nanyi sasa, Roho mliyemwona hapa usiku wa leo aliyejua siri za moyo, Roho yuyo huyo ananiambia kunao wengi hapa wanaopaswa kuja. Simameni sasa mje hapa na kusimama kuzunguka jukwaa hili dogo hapa kidogo kwa ajili ya maombi. Mtakuja? Mungu akubariki. Mungu akubariki, mama. Mungu abariki . . .

Usinipite, Ee mpole . . .

Waweza kuja, yeyote yule? Unaamini Mungu husikia maombi? Njoo na moyo mwaminifu.

Unapozuru wengine,
Usi- . . .

201 Shukeni kutoka kwenye roshani, sivyo? Baadhi yenu vijana kwenye kipindi muhimu cha maisha, njoni mkamkubali Kristo kama Mwokozi wenu. Mtafanya hivyo usiku wa leo? Mkajazwe na Roho Mtakatifu. Huu ndio wakati, mahali, kila kitu kiko tayari sasa. Hakutakuwako na udhuru, kwa kuwa Roho hasa aliye hapa usiku wa leo atasimama dhidi yako kwenye Siku ya Hukumu. Sasa, mnajua nisingesema mambo haya isipokuwa yawe hivyo. Shukeni kutoka kwenye roshani.

Mwokozi . . .

Kwa uchaji, utulivu, waweza kuondoka kitini mwako? Piga tu hatua chache, shuka uje hapa chini, usimame hapa kwa ajili ya maombi. Mungu awabariki hawa ambao wamekuja.

. . . kilio;
Unapo- . . .
Usinipite.

202 Nilisimama karibu na maskini msichana aliyekuwa akifa si muda mrefu uliopita, alikuwa kwenye mmoja wa mikutano. Akasema, "Usiombe, Ndugu Branham," akasema, "siku yangu imekwisha." Akasema, "Usiku mmoja kwenye mkutano wako ilikuwa ni vigumu kwangu kuketi kitini, nikiketi tu pamoja na mvulana mpenzi wangu. Nilimwuliza kama angekuja, akasema, 'La.'"

203 Lakini akasema, "Hiyo ilikuwa ndiyo siku yangu ya mwisho." Akasema, "Imechelewa kupita kiasi sasa." Msichana huyo, msichana mzuri, bali alikuwa akifa kwa ugonjwa wa zinaa wasingeweza kuukomesha. Naye mtayarisha mazishi, rafiki yangu, akamsukumia ma- . . . ugiligili wa kuufanya mwili usioze mwilini mwake. Kaendelea kusogea, wasingeweza kupata mahali ilipokuwa. Wakainusia. Mashimo yalikuwa yamekula ninii ya mwanamke huyo . . . mwili wa msichana huyo . . . msichana mrembo. Kasema, "Nilipaswa kuja."

204 Alikuwa ni mfuasi wa kanisa. Naam, bwana. Mchungaji wake amesimama pale, akivuta sigara wakati alipokuwa

akifa. Mnajua kile alichomwambia? “Ewe mdanganya watu. Uliniambia nilikuwa sawa; ulikosea.” Akasema, “Ninakufa na nimepotea, nawe ndiwe uliyesababisha hilo.”

205 Akamwita msichana ambaye huja kwenye Maskani ambaye alijaribu kumwongoza kwa Kristo. Wote wawili walienda kwenye shule ya sekondari ya juu pamoja. Akajaribu kumfanya aje; bali ilikuwa imechelewa sana, msichana huyo alikuwa amekufa kabla yeye kufika kule. Alitaka kutubu. Alitaka, kumwomba msichana huyo msamaha, maana alikuwa amemwita jina baya: “mtakatifu anayejibingirisha.”

206 Sikuzote hutambulika mwishoni mwa safari. Hapo ndipo unapofanya kongamano lako na malaika wa mauti. Anamjia kila mmoja wenu. Utakutana naye moja ya asubuhi hizi. Unaweza ukakutana naye kwenye barabara kuu usiku wa leo. Huenda ukakutana naye kitandani mwako usiku wa leo. Utakutana naye mahali fulani, nawe utafanya kongamano. Anavizia karibu sasa. Malaika wa Mungu wanavizia karibu. Utawataka waitetee kesi yako kwenye siku hiyo. Wanazungumza sasa, hivi hutakuja? Mara nyingine tena tunapongojea.

Natumaini tu ustahilifu Wako,

Usilitumainie kanisa lako, tumainia ustahilifu Wake.

. . . tafuta uso Wako;
Iponye roho yangu iliyojeruhiwa, na kuvunjika,
Niokoe kwa neema Yako.

Mwokozi, Mwokozi,
Sikia ninii langu nye- . . .

Wafanya kazi wa binafsi, mwaweza kuja sasa?

Unapozuru wengine,
Usipite . . . ( . . . ? . . . )

Mwokozi . . .

207 Wakati wafanya kazi wa binafsi wanapokuja, kila mmoja akija huku, wanawake na waende kwa wanawake, wanaume kwa wanaume. “Njoni sasa, haya tusemezane,” asema Bwana. “Dhambi zako zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji.”

Usinipite.

Mwokozi, Mwokozi,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

. . . mimi kwenye kiti Chako cha rehema
Nipate faraja tamu;

Hivi hamtatoka sasa? Njoo. Mtu fulani aje? Kunaye mwingine angetaka kuja kabla hatujaibadilisha ibada hii?

Mwokozi, Ee Mwokozi,
Loo, sikiliza kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Loo, usinipite.

208 Sasa, ni wangapi humu ndani wangetaka kuyaweka maisha yao wakfu upya kwa Kristo? Inua mkono wako. Sema tu, "Tangu usiku huu, na kuendelea, kwa msaada wa Mungu, nitayaweka maisha yangu wakfu kwa Mungu." Inueni mikono yenu, Wakristo wote waaminifu. "Nitayaweka wakfu tena maisha yangu kwa Mungu."

Wote walio wagonjwa, inueni mikono yenu na kusema, "Nitamwamini Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji wangu sasa. Nitamwamini."

Ninaamini Baba yetu wa Mbinguni anafurahishwa na hao watu wanaokuja kumpokea Kristo. Si mnaamini hivyo?

209 Sasa, sote na tusimame kwa miguu yetu kwa muda kidogo tu, hao jamaa ambao wanaweza, kwa ajili ya ibada yetu ya kujiweka wakfu, kujiweka wakfu upya kwa Mungu. Na tusimame sasa kufanya upya nadhiri zetu na kujiweka wakfu kwetu kwa Kristo. Mnampenda? (Vema, ubadilishe wimbo, ukipenda, kwa wimbo, "Nampenda, Nampenda.")

Nampenda . . .

Kila mmoja, sasa, kila mtu pamoja.

Nampenda, Na . . .

Sasa jiweke wakfu Kwake.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu . . .

210 Sasa, kila mmoja inamisha kichwa chako sasa, na katika maombi ya kujiweka wakfu jitolee mwenyewe kwa Kristo, wakati nitakapomwomba mmoja wa hawa wahudumu hapa, kama atakuja na kuomba maombi ya kujiweka wakfu; papa hapa ndugu, ukipenda. Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu tunapoomba.

61-0410 Makongamano
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org